**WAGANGA** kienyeji wafunga barabara, wadhibitiwa kwa mabomu ya machozi

UKURASA 2

**KATIBU** Mkuu mpya awaweka kitanzini vigogo kwa upotevu wa maji unaotisha

UKURASA 2



**KESI** ya Gekul yaanza tena mahakamani

UKURASA 19


# Nipashe

Jumanne Machi 19, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JA...

ISSN 0856 • Na. 0581620

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
Maoni@nipashe.co.tz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




**GIROUD KUMFUATA MESSI MAREKANI**

UKURASA 22

## MIAKA 3 YA SAMIA

# Mabosi wenye dhamana wasimulia mchakamchaka

Ukurasa wa 2, 3, 4, 5, 7, 8, 11, 12, 13 & 14



Rais Samia Suluhu Hassan akiapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Machi 19, 2021.
**PICHA: MAKTABA**



UKURASA WA 24

## GAMONDI NA HALI YA PACOME, YAO MECHI MAMELODI

LICHA ya kupoteza pointi tatu mbele ya Azam FC juzi katika mechi ya Ligi Kuu Bara kwenye Uwanja wa Benjamin...

## Mapya yaibuka msaada chakula kutoka Marekani

UKURASA 4




MIAKA 3 YA UBORA



Mhe. **Dr. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Salamu za Pongezi**

Bodi ya Wakurugenzi, Mkurugenzi Mkuu, Menejimenti pamoja na Wafanyakazi wa **Bharya Engineering and Contracting Company Limited** , tunaungana na Watanzania wote kupongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Dr. Samia Suluhu Hassan** kwa kutimiza miaka mitatu ya ubora ofisini kwa utendaji na uwajibikaji wake katika kusimamia na kutekeleza yale aliyoyaahidi ndani ya kipindi hiki cha miaka mitatu. Pia tungependa kumshukuru MH. Mama wa Taifa kwa kufungua milango ya biashara kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia kujenga mahusiano bora kwenye biashara na amani.
Tunamuombea afya njema na tuko pamoja katika kuhakikisha agenda ya maendeleo ya Watanzania inafanikiwa.

TUNAKUTAKIA KILA LA HERI KWENYE MIAKA IJAYO !
RAMADAN KAREEM!

BECCO


**MICHEZO** **SIMBA, YANGA KUVAANA Z'BAR** UK. 24 **KATUNI** UK. 6

MIAKA 3 YA SAMIA

# Mabosi wenye dhamana wasimulia mchakamchaka

**Na Mwandishi Wetu**

LEO Rais Samia Suluhu Hassan anatimiza miaka mitatu tangu alipoapishwa kushika wadhifa huo Machi 19, 2021 baada ya kufariki dunia Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli Machi 17, 2021.

Viongozi mbalimbali wa serikali, wakiwamo mawaziri, wameeleza mavuno ya uongozi wa Rais Samia na walivyokabiliana na 'mchakamchaka' wake kiutendaji.

Naibu Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko, jana aliagiza kuanzishwa kitengo cha nishati safi ya kupikia ili kutekeleza ajenda ya Rais Samia kufikia asilimia 88 ya wanawake wanaotumia nishati hiyo ifikapo mwaka 2030.

Pia aliagiza matumizi ya gesi asilia kupewa kipaumbele ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma na kuachana na kuandaa na kushiriki makongamano ya masuala hayo bali kuingia kwenye utekelezaji kwa vitendo.

Dk. Biteko ambaye ni Waziri wa Nishati aliagiza hayo wakati akifungua mkutano wa tano wa Baraza la Wafanyakazi la Wizara ya Nishati wenye lengo mahususi la kupitia na kupitisha rasimu ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2024/25.

"Rais Samia Suluhu Hassan ndiye kinara wa utekelezaji ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia Afrika, hivyo wizara lazima iweke mkakati wa kitaasisi na kimfumo kwa ajili ya kufanikisha ajenda hiyo, ili utekelezaji suala hili usiwe ni jambo la zimamoto," alisema Dk. Biteko.

Alisema wizara hiyo ina jukumu la kuihamisha nchi kutoka matumizi ya mafuta na kuhamia kwenye matumizi ya gesi (CNG) kwa kutengeneza mazingira ambayo yatapunguza utegemezi wa mafuta na hivyo kufanya nchi kujiendesha kwa kutumia CNG.

Aliagiza watendaji wa wizara kusimamia pia utekelezaji suala hilo huku akiwataka kufanya kazi kwa bidii huku wizara ikiangalia stahiki zao ikiwamo motisha.

Alisema kuwa watumishi wana deni la kutumikia Watanzania kwa kuwa wamepewa dhamana ya kusimamia Sekta ya Nishati kwa niaba yao hivyo watimize wajibu huo.

Pia aliwataka wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Nishati kupitia bajeti hiyo kwa umakini kabla haijafika katika ngazi ya Kamati ya Bunge na baadaye katika Bunge la Bajeti.

Awali, Mwenyekiti wa Baraza hilo, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba, alisema kuwa baada ya baraza kupitisha Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2024/25, hatua inayofuata ni kupitishwa kwenye Kamati za Bunge na baadaye Waziri wa Nishati ataisoma bungeni kwa ajili ya kupitishwa na Bunge.

Kuhusu bajeti ya mwaka 2023/24, Mramba alisema masuala

yaliyopangwa kufanyika kwenye bajeti hiyo yametekelezwa kwa kiasi kikubwa, hivyo kutoa mwanga kuwa bajeti ijayo kutekelezwa vizuri.

Aliongeza kuwa kwa sasa sekta ya nishati inatazamwa upya kwa kuangalia mchango wa nishati jadidifu katika sekta, nishati bora ya kupikia, uhifadhi wa nishati na matumizi bora ya nishati, lengo likiwa kuiboresha zaidi sekta husika kwenye nyanja mbalimbali.

***SOMA MAKALA NA MATANGAZO KUHUSU MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA UK. 3, 4, 5, 6, 7, 8, 11, 12, 13 & 14**



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (katikati) akizungumza na viongozi wa Benki ya NMB wakiongozwa na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi (kulia) baada ya kushiriki jukwaa la kuelezea mafanikio ya Wizara ya Kilimo katika kipindi cha miaka mitatu ya serikali ya awamu ya sita, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Katibu Mkuu mpya awaweka kitanzini vigogo upotevu maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RIPOTI ya utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini kwa Mwaka 2022/23 imebaini kuwapo vikwazo vinane vinavyozikabili mamlaka hizo, ikiwamo kuongezeka upotevu wa maji, hali inayosababisha kukosa mapato.

Kutokana na hilo, Katibu Mkuu mpya Wizara ya Maji, Mwajuma Waziri amesema atachukulia hatua dhidi ya mamlaka ambazo utendaji wake hauridhishi kwa kuwa na kiwango kikubwa cha upotevu huo na kusuasua kwenye ukusanyaji mapato.

Akizindua ripoti hiyo iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) jijini hapa jana, Mwajuma alisema upotevu wa maji dhidi ya kiwango cha maji kinachozalishwa umeongezeka kutoka asilimia 35.5 mwaka 2021/22 hadi kufikia asilimia 37.2 mwaka 2022/23.

"Hii haikubaliki hata kidogo. Sote tunajua kiwango cha upotevu wa maji kinachokubalika ni chini ya asilimia 20. Ni lazima mamlaka za maji ziweke na kutekeleza mikakati ya kuhakikisha zinapunguza kiwango cha upotevu wa maji," alionya.

Alizitaka mamlaka hizo kuzingatia miongozo mbalimbali ya kudhibiti upotevu wa maji ambayo hutolewa na EWURA kama vile Mwongozo wa Kupunguza Upotevu wa Maji wa Mwaka 2021 ambao unazitaka mamlaka za maji kuandaa mizania ya kupima viwango vya upotevu maji kwa mujibu wa Mwongozo wa Jumuiya ya Kimataifa ya Wataalamu wa Maji (IWA).

"Mamlaka za maji pia zinapaswa kuzingatia mwongozo wa kuchagua, kufunga, kupima na kufanyia matengenezo Dira za Maji kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2021 ili kudhibiti upotevu huu wa maji," alisema.

Kuhusu kuzorota ukusanyaji mapato, Katibu Mkuu alisema ripoti inaonesha kushuka kwa jumla ya mapato yaliyokusanywa kutokana na huduma ya majisafi na majitaka na shughuli nyingine za mamlaka kwa takribani asilimia mbili kutoka Sh. bilioni 401.48 mwaka 2021/22 hadi kufikia Sh. bilioni 393.34 mwaka 2022/23.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile, alisema ripoti hiyo ni ya 15 na mamlaka 85 zimefanyiwa tathmini ambapo pamoja na kuimarika kwa utendaji kazi, uchambuzi umebainisha vikwazo vinane vinavyozikabili ikiwamo kutokidhi kiwango cha dawa katika maji yanayosambazwa, majitaka yaliyotibiwa kutokidhi viwango vya ubora kwenye viashiria vya mahitaji ya oksijeni kibaiolojia na kikemikali.

Pia alisema uwiano mdogo wa idadi ya watu wanaopata huduma ya majisafi na usafi wa mazingira, uhaba wa miundombinu ya kutibu majitaka na topetaka kinyesi; uwiano mdogo wa uzalishaji maji kulinganishwa na mahitaji; bei za maji za muda mrefu ambazo haziendani na gharama halisi za uendeshaji na upatikanaji wa huduma isiyotosheleza ya usafi wa mazingira.

## Waganga wa kienyeji wafunga barabara

**Na Beatrice Shayo**

MABOMU ya machozi yametumika kutawanya waganga wa kienyeji, maarufu kwa jina la lambalamba, waliokuwa wamefunga barabara kwa zaidi ya saa tatu kwa kuweka miti na mawe katika eneo la Mtumbatu, mpakani mwa Gairo na Kilosa.

Ni tukio hilo la juzi saa saa nne usiku, waganga hao walipofunga barabara, wakishinikiza Mwenyekiti wa Kijiji cha Mtumbatu na mzee wa mila kuachiwa baada ya wawili hao kushikiliwa na polisi na kutaka kuruhusiwa kufanya kazi zao za lambalamba.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, alisema wanalaani kitendo hicho cha kutaka kuleta taharuki na uvunjifu wa amani.

"Kitendo cha kufunga barabara hii kubwa ni kututengenezea taharuki ambayo haina sababu na wala haina msingi. Hii ni njia kuu ya usafirishaji inayounganisha mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na mikoa ya pembeni na hata nchi za jirani. Ni kutaka kutikisa uchumi wa nchi yetu.

"Ninadhani mmeona dakika tano ukifunga barabara picha unayoipata ni kwa namna gani unaweza kutikisa uchumi wa nchi kwa namna moja ama nyingine. Hiki kitendo kilichofanywa si cha kiungwana," alisema.

Shaka alisema kikundi cha watu wachache kilitaka kuhamasisha imani za kishirikina kutoka kwenye mfumo wao binafsi na kufanya kuwa mfumo ndani ya jamii.

"Mnatumbia walikubaliana kuwa watoto shuleni wanaanguka, waletwe waganga hao lambalamba kuwafanyia tiba, lakini taarifa zilizopo ni kwamba wameshazunguka kwenye jamii nzima na kuletea uchonganishi, uvunjifu wa amani, taharuki na kubwa kuliko lote wanaweza kutusababishia maafa makubwa," alisema Shaka.

"Ina maana hawa hawakuja kwa ajili ya shule kama inavyodaiwa, kwanini tuwachangishe wazee kwa lazima Sh. 10,000? Kwanini tuchukue madebe ya watu ya mahindi? Nani aliyetoa hicho kibali? Ni mwenyekiti wa kijiji au ni nani? Kama ni huyo mwenyekiti, amekosea kutoa kibali," alisema Shaka.

Shaka alisema maelekezo ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, ni wilaya zote mbili kuendelea kulinda amani na usalama.

Awali, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mahemu, Agnes Lutambi, alipatiwa taarifa ya watoto kuanguka shuleni na kuelezwa waliitwa viongozi wa dini ikashindikana, wakaona itumike njia ya kuita waganga ili kutatua tatizo hilo.

"Walivyotuletea huo, muktasari tuliwajibu sisi kama serikali hatuamini hao waganga, tutakachokifanya ni kutatoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa shule na kuwapo walimu katika hiyo shule, lakini baadaye ofisa wa polisi alinitafuta na kuja kijiji kunihoji nikamweleza tatizo, usiku ninapatiwa taarifa wamefunga barabra," alisema.

Diwani wa Mtumbatu, Amani Sewando, alisema ameshangazwa kuona matibabu ya aina hiyo katika kijiji cha karibu, wananchi wanachangishwa kila nyumba Sh. 10,000 au madebe mawili ya mahindi.

"Nikaona wananchi wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa, hawa watu wameanza kuchangisha kila nyumba Sh. 10,000, yupo huyu mama wa viti maalum naye kachangishwa katika nyumba yake, nikasema hili jambo halipo sawa, nikatoa taarifa polisi, nikiwa njiani ninaambiwa waganga wameziba barabara kubwa, magari hayawezi kupita na kusababisha foleni kubwa," alisema.

Kwa mujibu wa Shaka, hadi jana jioni, Jeshi la Polisi lilikuwa linawashikilia watatu kuhusiana na suala hilo. Hao ni Willian Msagala (71), Falesi Mwanamasi (63) na Andrea Ndahani (38).

TOLEO MAALUM

# Miaka mitatu ya kuondoa giza mijini, vijijini



Mkurugenzi TANESCO Eng. Gissima Nyamo - Hanga



Viongozi wengine walioambatana na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ni Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Naibu Katibu Mkuu Mteule Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga, Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO, Dkt. Rhimo Nyansaho na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mhandisi Gissima Nyamo-Hanga

*Na Mwandishi Wetu*

MIAKA mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, madarakani, imechochea utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya umeme ambayo inalenga kuiondoa Tanzania gizani; na kuwa na mipango ya kuuza nishati hiyo nje ya nchi.

Mradi wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP), unaolenga kuzalisha megawatt 2115, tayari umeanza kazi na kupunguza mgawo wa umeme kwa asilimia 85.

Hii ni baada ya mwezi uliopita, serikali kuingiza megawati 235 kwenye gridi ya Taifa baada ya kuwasha mtambo namba tisa.

Mwishoni mwa mwezi uliopita, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dotto Biteko, alisema kwasasa upatikanaji wa umeme ni asilimia 85 na kwamba mgawo umepungua na utakwisha siku za karibuni.

Taarifa zinaonesha kwamba Rais Samia alipoingia madarakani mwaka 2021, aliukuta mradi huo ukiwa asilimia 33 ya utekelezaji tangu ulipoanza kujengwa mwaka 2015.

"Amehakikisha fedha zinapatikana na kulipwa kwa wakati kwa mkandarasi... ninafurahi kusema kile nilichokuwa nimeahidi kwamba Februari 25, mtambo namba tisa unaingiza megawati 235 kimetimia. Hii ni kutokana na msukumo mkubwa. Kwa ratiba tuliyokuwanayo ya kawaida umeme huu ungefikia mwezi wa sita ila kwa msukumo mkubwa wa Rais Samia tumefanikisha," alisema Biteko.

Kabla ya kuwashwa kwa mtambo huo, nchi ilikuwa inakabiliwa na upungufu wa megawati 200 hadi 400 na kwamba matarajio ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuondoa mgawo mwishoni mwa mwezi huu.

"Nafurahi kuwaambia Watanzania uwekezaji umejibu, tumepata umeme pamoja na siasa nyingi na magumu tuliyopitia...jambo muhimu Watanzania wanataka umeme hawataki maneno, tumechagua kutenda zaidi kuliko kusema," alisema.



Mradi wa Julius Nyerere hydroelectric power plant (JNHPP)

Kwa mujibu wa Biteko, mahitaji ya umeme yanaongezeka na kwamba serikali imeongeza vyanzo vingine ili kuhakikisha umeme wa uhakika unapatikana.

Wachambuzi wanaeleza kuwa uwekezaji mkubwa unaoonekana kwenye sekta ya nishati ni kutokana na ndoto ya serikali kujenga uchumi wa viwanda.

Mathalani, katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia, Mkoa wa Pwani, umeshuhudia ongezeko la viwanda na kwamba hivi sasa 17 viko katika hatua ya mwisho ya ukamilishaji.

Mwezi uliopita, Mkuu wa mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alikaririwa akisema kuna viwanda 1,533 vikubwa, 120 vya kati na 124 vidogo ambavyo vinahitaji umeme wa uhakika.

Mradi wa JNHPP una thamani ya Sh. trilioni sita ukitegemewa kuzalisha megawati 2,115 za umeme utakapokamilika.

Mradi wa JNHPP unaoshika nafasi ya kwanza kwa ukubwa katika miradi yote inayotekelezwa katika nchi za Afrika Mashariki na ni wa nne kwa miradi yote inayotekelezwa Afrika.

Mradi unaoshika nafasi ya kwanza Afrika ni wa Grand Ethiopian Renaissance Dam (6,400 MW) uliopo nchini Ethiopia, namba mbili ni ule wa Batoka George Hydroelectric Dam (2,400 MW), wa nchini Zambia katika Mto Zambezi na wa tatu ni mradi wa Caculo Cabaco Hydroelectric Dam (2,172 Mw) wa nchini Angola.

**IFAKARA SUBSTATION**

Agosti mwaka jana, kituo cha kupokea, kupoza na kusambaza umeme cha Ifakara (Ifakara substation), kilikamilika na hivyo kuzihakikishia umeme wa uhakika wilaya za Kilombero na Ulanga, mkoani Morogoro na hivyo kuondokana na adha ya kukatika kwa umeme.

**TAZA RUKWA**

Mapema mwaka huu, serikali ilieleza kupeleka umeme wa gridi mkoani Rukwa kupitia mradi wa TAZA, ulioanza kutekelezwa Novemba, 2023 unatarajiwa kukamilika Agosti, 2026, ikiwa ni jitihada za kuhakikisha maeneo yote nchini yanapata umeme wa uhakika.

**RUSUMO**

Huu ni mradi wa kuzalisha megawati 80 za umeme na unatekelezwa kwa pamoja na nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi ambazo zimeanza kupata nishati hiyo kutoka kwenye mradi huo.

Desemba mwaka jana, mawaziri wa nishati kutoka nchi hizo waliridhishwa na utekelezaji wake na wakakubaliana kwamba uzinduliwe mwezi huu na kumtaka mkandarasi kukamilisha mradi huo mapema na atoe cheti cha kukamilisha mradi.

Mradi wa umeme wa Rusumo utazalisha megawati 80 ambapo kila nchi itapata megawati 27.

**GRIDI IMARA**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa upande wake, limeweka saini mikataba sita kwa ajili ya miradi 26 ya kuimarisha gridi ya Taifa.

Mikataba sita ya kuimarisha gridi iliyosainiwa mwaka jana ililenga kujenga mradi mkubwa wa umeme wa kuimarisha Gridi ya Taifa ambao utaigharimu Sh. trilioni 4.42 ambao utakamilika ndani ya kipindi cha miaka minne.

Wachambuzi wanaeleza kuwa upatikanaji wa umeme wa uhakika unachangia ukuaji wa uchumi, uboresha huduma za jamii vijijini zikiwemo afya, elimu, maji safi, mawasiliano na usalama pamoja na kuhifadhi mazingira, kuimarisha usalama na kukuza ajira.






Picha za miradi na tanesco tukiwa kwenye matengenezo nikonekt call center nk

tanesco_official_page umemeforum.blogspot.com tanescoyetultd tanescoyetu

MIAKA MITATU YA SAMIA

# Ujangili wa tembo wafyekwa kwa 83%

Na Romana Mallya

UJANGILI wa tembo umepungua kwa asilimia 83 kutoka mizoga sita mwaka 2021/22 hadi mitatu mwaka huu wa fedha (2023/24) kutokana na kuimarishwa ulinzi, ari ya kazi miongoni mwa askari na kuongezezwa vitendea kazi.

Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka wa Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), Mabula Nyanda, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na wahariri na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya mamlaka hiyo katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Kamishna Nyanda alisema mafanikio katika kipindi hicho ni pamoja na kuimarika ulinzi wa rasilimali ya wanyamapori na malikale na kupunguza ujangili.

"Tatizo la ujangili wa tembo lilikuwa kubwa huko nyuma walikaribia kuisha, lakini tumefanikiwa kuimarisha ulinzi wao.

"Tumepunguza ujangili hususani wa tembo kwa asilimia 83 kutoka mizoga sita mwaka 2021/22 hadi mizoga mitatu mwaka 2023/24 (hadi Februari 2024) kutokana na kuimarika kwa ulinzi na kuongezeka kwa vitendea kazi.

"Pia morali ya watumishi imeongezeka, tumeimarisha mtandao wa intelijensia, doria za mwitikio wa haraka, matumizi ya teknolojia (GPS, ndege nyuki na kisukuma mawimbi)," alisema.

Kamishna Nyanda alisema TAWA ina jukumu kisheria kusimamia eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 133,276.36 zikijumuisha mapori ya akiba 28 (Km za mraba 104,176.36), tengefu 23 (Km za mraba 29,100) ya malikale ya Kinduchi, Kilwa-Kisiwani, Songomnara na Kisiwa cha Lundo.

Pia wana jukumu la kuzuia ujangili wa wanyamapori, kusimamia mashamba na bustani za wanyamapori za serikali na kutatua migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu.

Kamishna Nyanda pia alisema wanatekeleza mikataba ya kimataifa ya kikanda na kimataifa, ukiwamo wa usimamizi wa biashara ya wanyamapori na mimea inayotaka kutoweka.

Alitaja wanyama walio katika hatari ya kutoweka ni pamoja na faru, tembo, sheshe (wanapatikana Kilombero), mamba, chui na simba, ingawa simba na chui idadi yao bado ni kubwa nchini. Kamishna Nyanda pia alisema wamefanikiwa kupunguza migogoro kati ya hifadhi na wananchi hususani iliyohusu mipaka.

"Tumepunguza migogoro katika mapori ya akiba saba kati ya manane yaliyotolewa maelekezo na Kamati ya Mawaziri Wanane wa Kisekta. Tumeachia ekari 811,506 ambazo zimemegwa hifadhini na kupatiwa wananchi," alisema.

**WANYAMA WAKALI**

Kamishna Nyanda alisema kutokana na ongezeko la matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kati ya mwaka 2021/24, TAWA iliweka doria za siku watu 58,818 za usiku na mchana, wakikabiliana na matukio 8,001 katika wilaya 73.

Pia alisema wamejenga vituo 16 vya askari katika wilaya 16, pikipiki 50 zilizofungwa vifaa maalum zimenunuliwa na kutoa mafunzo kwa skauti wa hifadhi vijijini (VGS) na askari wa Jeshi la Akiba 184.

"Maeneo sugu yenye changamoto kubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu ni Bunda, Busega, Meatu, Same, Lindi, Korogwe Itilima, Liwale, Nachingwea, Mwanga na Tunduru," aliyataja.

Kamishna Nyanda alitaja mafanikio mengine ni pamoja na miradi ambayo TAWA inayafanya ikiwamo ujenzi wa Soko la Samaki Kilombero, shule na kuwezesha jamii kunufaika na uvuvi na ufugaji nyuki.

"Tumewezesha wananchi 7,511 kuvua samaki na 2,046, kufuga nyuki katika Mapori ya Akiba Rukwa, Ugalla, Uwanda, Moyowosi Kilombero na Inyonga," alisema.

Alitaja mafanikio mengine ni ongezeko la gawio la wanufaika kutoka Sh. bilioni 1.98 mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni 11.59 mwaka 2022/23.

"Pia kuna ongezeko la watalii wa picha kutoka 37,686 mwaka 2020/21 hadi 166,964 mwaka 2022/23 na watalii 116,529 kufikia Februari 2024.

"Tumeshuhudia pia ongezeko la idadi ya meli za kimataifa za utalii. Kati ya mwaka 2021/22 hadi 2023/24, idadi ya vitalu vya uwindaji vyenye wawekezaji imeongezeka kutoka 59 hadi 68.

"Vitalu 68 vimeuzwa Dola 8,277,000 kulinganisha na Dola 2,405,000 endapo vingeuzwa kwa njia ya utawala, ikiwa ni ongezeko la Dola 5,872,000, sawa na ongezeko la asilimia 224. Kila mwaka, kwa vitalu saba tutakuwa na uwezo wa kuingiza Sh. bilioni 15," alisema.

Kamishna Nyanda alisema katika uboreshaji na ufanisi wa utendaji kazi, wamenunua magari 60, boti za doria saba na za utalii mbili zenye uwezo wa kubeba abiria 30 na 60.

Kuhusu changamoto, Kamishna Nyanda alitaja suala la wanyamapori wakali na waharibifu kama tembo, mamba, kiboko na fisi ambao huathiri maisha ya wananchi. Ni matukio yaliyoongezeka na ni mtihani kwao, lakini wanaendelea kupambana.

Alisema waliweka mkakati wa kutoa elimu kwa jamii kuhusu njia za kujihami, wakiwa na mikakati mingine ya muda mrefu inayojumuisha mpango wa matumizi bora ya ardhi.

"Ugonjwa hatari kwa wanyamapori ni kimeta. Hili ni tatizo na changamoto kwetu. Kwa mwaka, idadi ya wanyama wanaotakiwa kuwindwa inategemea na takwimu za sensa na ndipo waamue idadi ya watakaowindwa.

"Kwa Tanzania, tunaruhusiwa kuwinda tembo 50 tu kwa mwaka kwa kuwa waliathirika sana kwa ujangili. Na tumeweka masharti magumu sana ya kuwawinda kama vile urefu sentimeta ngapi na kilo ngapi. Kama ukimpiga tofauti na viwango vilivyoainishwa ni shida, faini yake ni kubwa mno.

"Kila mnyama ana idadi yake katika uwindaji. Hata mamba wana idadi kukingana na mkataba wa kimataifa tuliouridhia kama nchi. Na kuna wanyama kama faru kwa sasa hakuna kibali. Twiga hakuna rukhsa ya kuwawinda kwa sababu wanatumika kama nembo ya taifa," alisema.

Kamishna Nyanda pia alitoa ufanunuzi kuhusu uchimbaji madini katika mapori ya akiba na tengefu, akisema kibali kilichotolewa ni kwa madini ya kimkakati, wakianza na madini ya urani kwenye Pori la Akiba Selous.

Pia alisema kwa sasa utekelezaji wa miradi ujenzi wa miundombinu ya reli na barabara zinazopita hifadhini, unazingatia uhai na uendelevu wa ikolojia ya hifadhi; barabara zinapitishwa juu na reli inapitishwa juu au katika mahandaki.



## Mapya yaibuka msaada chakula kutoka Marekani

Na Halfani Chusi

WAKATI Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe akipinga msaada wa chakula kutoka Serikali ya Marekani kwamba nchi inacho cha kutosha na virutubisho viwekwe mbele ya macho ya Watanzania, Shirika la Viwango Tanzania (TBS), limeibuka na kusema chakula hicho kilifuata taratibu za uingizwaji na ni salama kwa matumizi.

Juzi, Waziri Bashe akizungumzia mafanikio ya Rais Samia Suluhu Hassan katika sekta ya kilimo kwa miaka mitatu, alisema ameona kwenye mitandao ya kijamii mjadala mkubwa kuhusu kupewa chakula cha msaada.

Akipinga hoja hiyo Bashe alifafanua kwamba chakula hicho ni mradi unaofanywa na Shirika Lisilo la Kiserikali (NGO) katika shule za msingi na sekondari.

"Sisi tuliiambia ile NGO, kwamba nchi hii mchele upo na maharage yapo, zile pesa wanazozitumia kuwapa wakulima wa Marekani wawape wakulima wa Tanzania tununue hizo bidhaa kutoka hapa halafu hivyo virutubisho wanavyotaka kuweka wawekee hapa hapa Tanzania wakati sote tunaona," alisema Bashe.

Siku moja baada ya kauli hiyo ya waziri, TBS kupitia taarifa yake kwa vyombo vya habari iliyotolewa Machi 17, mwaka huu na Meneja Uhusiano na Masoko, Gladness Kaseka, imesema chakula hicho kilipofika kilifanyiwa ukaguzi na uchunguzi wa kimaabara na kuthibitika kuwa ni salama kwa matumizi.

Sehemu ya taarifa hiyo ilisema "Hivi karibuni kumekuwapo na taarifa iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusiana na msaada wa chakula (mchele uliongezwa virutubisho, mafuta ya kupikia, alizeti na maharage).

"Ambao ulileltwa na Wizara ya Kilimo ya Marekani kwa kushirikiana na Taasisi ya Jumuiya za Kimataifa katika baadhi ya shule za mkoa wa Dododma chini ya mpango uitwao 'pamoja tuwalishe" ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema TBS inapenda kuujulisha umma kuwa chakula hicho kilifuata taratibu za uingizwaji kilipofika kilifanyiwa ukaguzi na uchunguzi wa kimaabara na kuthibitika kuwa ni salama kwa matumizi.

Taarifa hiyo ilifafanua kwamba utaratibu wa kuongeza virutubishi kwenye chakula unakubalika kitaalamu na hufanyika kwa lengo la kuboresha lishe ya walaji.

"TBS inaendelea kusimamia kikamilifu jukumu la kuhakikisha chakula kinachoingia nchini kinakidhi vigezo vya usalama na ubora kwa muujibu wa matakwa ya viwango, ili kuendelea kulinda afya za walaji.

"Tunawashukuru wananchi ambao wanaendelea kutoa ushirikiano kwani suala la udhibiti wa usalama na ubora wa bidhaa ni mtambuka," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Machi 15, 2024 Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania, kupitia ukurasa wake wa mtandao wa X, zamani Twitter, ulitangaza msaada wake uliotoa kwa shule moja huko jijini Dodoma chini ya mpango wa ubalozi huo uitwao 'Tuwalishe Pamoja.'

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, msaada huo unajumuisha mchele ulioongezwa virutubisho, maharage na mafuta ya alizeti ambavyo vyote ubalozi ulisema vinatoka kwa wakulima wa Marekani.

TANGAZO

# MAFANIKIO YA SEKTA YA USHIRIKA KATIKA MIAKA MITATU (2021/2022 - 2023/2024) YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA



*Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan*

Tume ya Maendeleo ya Ushirika ni Idara ya Serikali inayojitegemea iliyo chini ya Wizara ya Kilimo iliyoanzishwa kwa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 ili kutekeleza majukumu ya Udhibiti na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika pamoja na Uhamasishaji wa Maendeleo ya sekta ya Ushirika nchini.

Majukumu makuu ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika ni pamoja na: Kuandikisha na kufuta vyama vya ushirika; Kukagua na Kusimamia vyama vya ushirika; Kutunza na kuboresha rejista ya vyama vya ushirika; Kutatua migogoro na malalamiko katika vyama vya ushirika; Kuhimiza na kuhamasisha maendeleo endelevu na ya kiuchumi ya vyama vya ushirika; Kutoa elimu na mafunzo kwa wanachama na watumishi wa vyama vya ushirika kuhusu uendeshaji wa ushirika; Kukusanya, kuhifadhi na kusambaza takwimu na taarifa za vyama vya ushirika; na Kufanya tafiti mbalimbali kwa maendeleo ya vyama vya ushirika.



*Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe (kulia), akimkabidhi vitendea kazi Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Abdulmajid Nsekela wakati wa uzinduzi wa Bodi mpya.*

**MAFANIKIO YA SEKTA YA USHIRIKA**

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Awamu ya Sita ya Serikali (2021/2022 - 2023/2024) inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Sekta ya Ushirika imepata mafanikio katika maeneo yafuatayo:

**1. Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika**

Tume imefanya kaguzi kwenye Vyama vya Ushirika ambapo imebainika kuwepo kwa kuimarika katika utendaji wa vyama vya ushirika kama inavyoonekana katika matokeo ya Kaguzi za mwaka wa fedha wa 2021/2022 na 2022/2023.

**Hali ya Kaguzi katika Vyama vya Ushirika**

| S/N | HALI YA UKAGUZI | 2021/2022 | 2022/2023 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Hati safi | 339 | 479 | (zimeongezeka kwa 41.30 %) |
| 2. | Hati zenye shaka | 2,393 | 2,475 | (zimeongezeka kwa 3.43%) |
| 3. | Hati isiyoridhisha na maoni | 1,198 | 127 | (zimepungua kwa 89.40%) |
| 4. | Hati mbaya | 2,075 | 830 | (zimepunguakwa 60%) |

Kuimarika kwa vyama kumechangiwa na jitihada za Tume kwa kuongeza vitendea kazi, ambapo hadi kufikia mwaka 2023/ 2024 Tume imenunua magari 15 katika Ofisi za Mikoa ukilinganisha na magari 7 yaliyokuwepo mikoani mwaka 2021/2022. Aidha, mafunzo kuhusu usimamizi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika yametolewa kwa Maafisa Ushirika katika mikoa 20, Watendaji wa Vyama vya Ushirika 7,517, Wanachama 40,253 na Viongozi 5,553.



*Baadhi ya magari yaliyonunuliwa na TCDC na kupelekwa katika Ofisi za Tume za mikoa kwa ajili ya Usimamizi na Uhamasishji wa Maendeleo ya Ushirika*

**2. Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Vyama vya Ushirika**

Katika kuimarisha uendeshaji wa Vyama vya Ushirika, Tume ilifanya zoezi la ukaguzi wa sifa za watendaji wakuu wa Vyama Vikuu vyote vya Mazao na Miradi ya Pamoja 50 na kubaini kuwa asilimia 35 tu ya watendaji wakuu walikuwa na sifa stahiki. Kupitia maelekezo ya Tume, Vyama Vikuu vinne (4) vya IGEMBENSABO, PMCU, ACU, na KICU vimeajiri watendaji wapya, na Vyama 11 vya KYECU, TAMCU, SORECU, CHUTCU, SORECU, TAMCU, MAMCU, TANECU, RIVACU, SIFACU na LATCU vimeomba vibali vya ajira kwa watendaji wake.

**3. Usimamizi wa Vyama vya Ushirika wa Kifedha (SACCOS)**

Tume katika kusimamia Vyama vya Ushirika vya kifedha (SACCOS), mafanikio yafuatayo yamepatikana; ambapo hadi kufikia Desemba 2023, mali za SACCOS ziliongezeka na kufikia Shilingi Trilioni 1.3 kutoka Shilingi Trilioni 1.22 mwaka 2022. Jumla ya Akiba na Amana zimeongezeka na kufikia Shilingi Billioni 980 kutoka Shilingi Billioni 897 mwaka 2022. Jumla ya Mikopo inayodaiwa imeongezeka na kufika Shilingi Trilioni 1.1 kutoka Shilingi Trilioni 1.05 mwaka 2022. Mtaji tete umeongezeka na kufikia Shilingi Billioni 214.7 na kutoka Shilingi Bilioni 203 mwaka 2022.

**Mafanikio ya SACCOS**

| Maelezo | Mwaka 2022 | Mwaka 2023 |
|---|---|---|
| | Shilingi | Shilingi |
| Mali za SACCOS | Trilioni 1.22 | Trilioni 1.3 |
| Akiba na Amana | Bilioni 897 | Bilioni 980 |
| Mikopo inayodaiwa | Trilioni 1.05 | Trilioni 1.1 |
| Mtaji tete | Bilioni 203 | Bilioni 214.7 |

**4. Vyama vya Ushirika kutumia mifumo rasmi ya masoko ya mazao ya wakulima**

Wakulima wameendelea kukusanya na kuuza mazao yao kupitia mfumo rasmi wa masoko kupitia Vyama vya Ushirika. Katika mwaka 2023/2024 hadi kufikia Machi 2024, jumla ya Tani 779,958 zenye thamani ya Shilingi 1,835,977,350,938 zilikusanywa na kuuzwa kupitia mfumo rasmi wa Ushirika ukilinganisha na Tani 597,298.58 zilizouzwa kwa thamani ya Shilingi 1,552,635,769,446 mwaka 2021/2022. Thamani ya mauzo imeongezeka kwa asilimia 18.25. Mazao yaliyouzwa kupitia Ushirika ni tumbaku, korosho, pamba, kahawa, ufuta, kakao, mkonge, chai, mbaazi, soya, zabibu, miwa na maharage.

**Thamani ya mazao yaliyouzwa kupitia Ushirika**

| Na. | | 2021/2022 | 2023/2024 |
|---|---|---|---|
| 1.! | Uzito kwa Tani | 597,298.58 | 779,958 |
| 2.! | Thamani (Shilingi) | 1,552,635,769,446 | 1,835,977,350,938 |




*Moja ya Minada ya mazao yanayouzwa kupitia Mfumo wa Ushirika na Stakabadhi za Ghala mkoani Mtwara.*

Aidha, kupitia Mfumo wa Mauzo ya Moja kwa Moja (Direct Sales), Vyama Vikuu vya Ushirika vya KCU (1990) Ltd na KDCU Ltd vya Mkoani Kagera, vimeendelea kuuza Kahawa Hai (organic coffee) katika Soko la Haki (Fair Trade Market). Hadi kufikia Februari 2024, jumla ya Kilo 4,813,850 za Kahawa Hai ambayo ilikuwa haijasagwa (coffee beans) na kahawa hai iliyosagwa (instant coffee), ziliuzwa kupitia Soko la Haki katika nchi za Ujerumani, Japani, Ubeligiji, Canada, China na Amerika ya Kaskazini kwa thamani ya Shilingi 30,576,880,548.90, ikilinganishwa na mauzo ya Kilo 1,797,722 zenye thamani ya Shilingi 10,801,014,641.00 zilizouzwa mwaka 2022/2023.

**Mauzo ya Kahawa hai iliyouzwa na vyama vya KDCU NA KCU**

| BIASHARA YA KAHAWA HAI KATIKA SOKO LA HAKI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| AINA YA KAHAWA | 2022/2023 | | 2023/2024 | |
| | KG | THAMANI(TSH) | KG | THAMANI(TSH) |
| ISIYOSAGWA | 1,612,540 | 10,391,207,760.00 | 4,640,400 | 30,162,013,29 8.90 |
| ILIYOSAGWA | 185181.6 | 409,806,880.80 | 173,450 | 414,867,250.00 |
| JUMLA KUU | 1,797,722 | 10,801,014,641.00 | 4,813,850 | 30,576,880,548.90 |

**5. Upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo kupitia Vyama vya Ushirika**

Katika msimu wa 2023/2024, jumla ya pembejeo zenye thamani ya Shilingi 307,673,032,600.00 zilinunuliwa kupitia Vyama vya Ushirika na kusambazwa kwa wakulima ikilinganishwa na pembejeo zenye thamani ya Shilingi 9,010,403,964.00 kwa mwaka 2021/2022. Aina za pembejeo zilizonunuliwa na kusambazwa kwa wakulima ni mbolea, viuatilifu (madawa), vifungashio, mbegu na miche kwa ajili ya mazao ya kahawa, pamba, korosho, mahindi, ufuta, alizeti, tumbaku na mpunga.

Aidha, katika mwaka 2023/2024, Vyama 776 vilipata vibali vya kununua na kusambaza mbolea kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), ikilinganishwa na Vyama 22 katika mwaka 2021/2022.

**Usambazaji wa Pembejeo**

| USAMBAZAJI WA PEMBEJEO KUPITIA VYAMA VYA USHIRIKA | | |
|---|---|---|
| PEMBEJEO | Thamani ya Mauzo (Shilingi) | |
| | 2021/2022 | 2023/2024 |
| MBOLEA | 6,018,386,364.00 | 12,178,621,500.00 |
| MBEGU na VIUATILIFU | 860,645,250.00 | 285,882,871,035.00 |
| VIFUNGASHIO | 2,050,135,850.00 | 9,328,015,550.00 |
| MICHE | 81,236,500.00 | 283,524,515.00 |
| JUMLA | 9,010,403,964.00 | 307,673,032,600.00 |

**6. Viwanda vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika**

Vyama vya Ushirika vinamiliki jumla ya viwanda 328; kati ya viwanda hivyo, viwanda vinne (4) vya kuchambua na kuchakata Pamba vya KACU Ltd (Shinyanga), MBCU Ltd (Geita), CCU Ltd (Chato) na SOLA (SIMCU Ltd Simiyu) vimefufuliwa ili kuongeza thamani na bei ya zao hilo katika soko. Aidha, viwanda viwili (2) vya kuchakata kahawa vimefanyiwa matengenezo, KDCU LTD (Kagera) na WAMACU LTD (Mara); na viwanda vipya vitatu (3) ambavyo ni vya kiwanda cha kukamua mafuta ya Mbegu cha Chama cha RUNALI, Kiwanda cha vifungashio cha SONAMCU na Kiwanda cha kubangua korosho cha TANECU LTD vimekamilika mwaka huu 2024.

**7.Ajira katika Vyama Vya Ushirika**

Kuimarika kwa Vyama vya Ushirika kumefanikisha kuongezeka kwa wananchi walioajiriwa katika vyama hivyo kufikia 153,982 mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na wananchi 100,100 waliopata ajira katika vyama mwaka 2020/21, ikiwa ni ongezeko la asilimia 53.8.

**8. Kukuza matumizi ya TEHAMA katika Vyama vya Ushirika**

■ **Matumizi ya MUVU**

Tume ya Maendeleo ya Ushirika imetengeneza Mfumo wa kidigitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) ambao ulizinduliwa mwezi Julai 2023. Lengo la MUVU ni kuimarisha usimamizi, kuboresha ufanisi na kurahisisha upatikanaji wa takwimu sahihi kwa ajili ya mipango mbalimbali ya maendeleo katika kukuza sekta ya Ushirika kwa ujumla.

Hadi Machi 2024, vyama vya ushirika 6,134 vimesajiliwa kwenye MUVU kati ya vyama 7,468 vilivyo kwenye Daftari la Usajili wa Vyama, na jumla ya Vyama 1,843 vimeanza kutumia MUVU katika shughuli za uendeshaji. Aidha, jumla ya Mali 9,106 za Vyama Vikuu vya Ushirika zenye thamani ya Shilingi 2,023,167,983,761 zimefanyiwa utambuzi na kuingizwa kwenye MUVU.

Mfumo huu umeunganishwa na Mifumo mingine mitano (5) ambayo ni Mfumo Mkuu Unganishi wa Serikali (GovESB), Mfumo wa Mizani ya Kielekroniki ya Upimaji wa Mazao (Mkulima Hub), Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Rasilimali (ERMS), Mfumo wa Ukusanyaji wa Malipo ya Serikali Kielektroniki (GePG) na Mfumo wa Usajili wa Watu kwa njia ya Mtandao chini Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).



*Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, akizindua Mfumo wa kidigitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU)*

■ **Mizani za Kidigitali**

Tume imesimamia mchakato wa upatikanaji wa Mizani ya Kidijitali kwenye vyama vya ushirika ambapo jumla ya Mizani za Kidijitali 1,178 zenye thamani ya Shilingi 3,534,000,000.00 zilinunuliwa na kusambazwa kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) vinavyojishughulisha na mazao ya kahawa, korosho, ufuta, soya, mbaazi, kakao na tumbaku katika Mikoa ya Kagera, Lindi, Mbeya, Tabora, Mtwara, Ruvuma na Pwani.



*Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde, akizindua matumizi ya Mizani za Kidijitali katika ununuzi wa mazao ya wakulima mkoani Lindi*

**9. Kuhamasisha Uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika**

Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaendelea kuratibu uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika kwa kuhamasisha wadau mbalimbali kununua Hisa ili kupata Mtaji wa Shilingi Bilioni 20 unaohitajika kuanzisha rasmi Benki hiyo. Kupitia uhamasishaji uliofanyika, uwekezaji katika Hisa umeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 4.7 Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi kufikia Shilingi Bilioni 15.7 mwezi Februari, 2024 sawa na ongezeko la asilimia 236. Vyama vya Ushirika vitamiliki Hisa zote kwa asilimia 51 na Benki hiyo inatarajiwa kuzinduliwa rasmi ifikapo Mei, 2024.




**10. Kuvipanga Vyama vya Ushirika visivyo vya Kifedha kwenye Madaraja**

Katika kuviwezesha Vyama kujiendesha kibiashara, Tume imeanza mchakato wa kupanga vyama kwenye madaraja. Hadi sasa, Tume imeandaa kigezo cha kupanga Vyama katika madaraja. Kigezo hicho kimeweka madaraja matatu (Daraja A, Daraja B na Daraja C) kwa kutumia kigezo cha ukubwa wa mali. Lengo ni kuweza kutambua ukubwa wa chama na kuweka utaratibu bora wa kuvisimamia. Aidha, imetengeneza kigezo cha ufanisi kitakachogawa vyama kwenye madaraja 4 (Utendaji Bora; utendaji mzuri sana; utendaji wa kuridhisha na utendaji dhaifu). Upangaji vyama kwenye Madaraja utafanyika kwenye MUVU baada ya kuingizwa taarifa za utendaji wa vyama.

**11. Kujenga Taswira Chanya ya Ushirika (Branding of Cooperatives Model)**

- Tume imeandaa na kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano (Communication Strategy) na Mwongozo wa Mawasiliano kwa Tume na vyama kwa kufanya yafuatayo:
- Tume inatumia kikamilifu Mitandao ya kijamii (facebook, Instagram), tovuti na Vyombo vya Habari kuhabarisha umma kuhusu yanayotokea kwenye ushirika kila siku; Vyama vimeanza kutangaza mafanikio yake kupitia mikutano mikuu ya vyama kwa kushirikiana na Vyombo vya Habari. Aidha, baadhi ya vyama (kama vile TANECU, KACU, KDCU, WAMACU, RUNALI, SONAMCU, MAMCU, TAMCU, LINDI MWAMBAO,) na baadhi ya SACCOS ikiwemo BANDARI, TANESCO, NGOME, URA na KKKT - ND) na Benki ya Ushirika Kilimanjaro vimeanza kutumia Vyombo vya Habari na social media kutangaza shughuli zake; na
- Tume kwa kushirikiana na Vyama vya Ushirika inatangaza mafanikio ya Ushirika kwenye Majukwaa ya Ushirika ya kila mkoa na kilele chake kinafanyika kitaifa kwenye Siku ya Ushirika Duniani (SUD) na Maadhimisho ya Siku ya Ushirika wa Kifedha Duniani (ICUD).



*Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Banson Ndiege akizungumza na Waandishi wa Habari Jijini Dodoma*

**USHIRIKA – PAMOJA TUJENGE UCHUMI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Miaka mitatu ya Rais Samia kuna mengi ya kujivunia

**ALIPOAPISHWA** kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alikuja na kaulimbiu yake ya 'Kazi iendelee' kwa kuendeleza yale yaliyoachwa na Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Magufuli.

Kama Katiba ya nchi inavyosema, Rais aliyepo madarakani atakapokuwa amefariki dunia, anayestahili kushika madaraka hayo ni Makamu wake ambaye ni Samia Suluhu Hassan.

Kifo cha Magufuli kilishtua Watanzania wengi kwa kuwa ni mara ya kwanza kwa Tanzania Rais kufariki dunia akiwa bado madarakani.

Kabla ya kifo chake kutangazwa wananchi walitaka waelezwe wapi alipo Rais wao baada ya kusambaa taarifa kuwa ni mgonjwa na amelazwa hospitali.

Kila Jumapili alizoeleka kuonekana kanisani, Mtakatifu Petro (St. Peter's) Oysterbay, jijini Dar es Salaam, lakini baada ya kutoonekana Jumapili kadhaa waamini wenzake walianza kuingia wasiwasi na kuhoji wapi alipo Rais Magufuli.

Tanzania imeweka historia kwa kuwa na Rais wa kwanza mwanamke na pia kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Tangu alipoapishwa kushika madaraka hayo, Rais Samia hajatetereka, kwa sababu alishapata uzoefu wa kutosha wa kuwa na uhusiano na viongozi wa nchi zingine kutokana na kumwakilisha mara kwa mara Rais Magufuli katika safari za kikazi nje ya nchi na vile vile mikutano ya kimataifa ambayo ilimjengea ujasiri wa kujiamini.

Taarifa za kifo cha Rais Maguli zilitolewa kwa wananchi kupitia Televisheni ya Taifa na aliyetangaza ni Makamu wa Rais (Rais Samia) ambaye kwa wakati huo alikuwa mkoani Tanga kwenye ziara ya kikazi na huko huko ndiko alikotangazia taarifa hizo.

Katika kipindi chake hiki cha miaka mitatu, Rais Samia amefanya mambo mengi, kubwa likiwa la hali ya kisiasa kwa kudumisha demokrasia nchini baada ya kukubali kukaa meza moja na vyama vya upinzani na kuruhusu mikutano ya hadhara ya kisiasa ya vyama hivyo, ambayo awali ilizuiwa na iliyoruhusiwa ni ya ndani inayohusu masuala ya vyama vyao.

Kwa upande wa miundombinu, amefanya mambo makubwa kwa kuendeleza kazi iliyoachwa na mtangulizi wake, yakiwamo madaraja hasa linalokatika Selander kutoka Oysterbay hadi Hospitali ya Aga Khan, maarufu Daraja la Tanzanite.

Ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo linatarajiwa kuondoa kabisa tatizo la kukatika umeme mara kwa mara na kupata uhakika, umefikia hatua za mwisho mwisho na vile vile ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), ambao utarahisisha usafirishaji abiria na mizigo na kuokoa barabara za kuharibika mara kwa mara kutokana na mizigo mizito inayobebwa na malori.


Rais Samia amegusa sekta nyingi zikiwamo za kilimo, afya, elimu kuhakikisha wananchi wanafaidika na maendeleo ya nchi yao kwa kuwa na chakula bora, elimu bora na elimu bora kwa kujenga miundombinu inayorahisisha ufanyaji kazi.

Pia katika safu yake ya viongozi wanaomsaidia amejaribu kugusa wanawake wenye uwezo kushika nafasi za juu ili kufikia lengo la Umoja wa Mataifa la Maendeleo Endelevu la 50/50 kwa viongozi wanawake na wanaume.

Hivi karibuni, Rais Samia ameanzisha utaratibu wa kusikiliza kero za wananchi 'Sema na Rais' kwa kuweka utaratibu maalum kila mwezi, makao makuu, Dodoma na jijini Dar es Salaam ambapo hadi mwishoni mwa wiki amefanikiwa kusikiliza malalamiko zaidi ya 13,000.

Utaratibu huu unamsaidia Rais kuwa karibu na wananchi wake na kusikiliza malalamiko yao wakiwa huru.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Christina Mwakangale

## Muungwana Lazima Nilonge

# Urais wake Samia, 'kamshika mama na mwana' hawaachii

**NAUNGANA** na Watanzania kulitakia mafanikio taifa letu, pia kumwombea afya njema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika safari yake ya kuendelea zaidi kuwatumikia wananchi, baada ya kuwaongoza kwa miaka mitatu.

Afya na elimu ni mambo ambayo naweza kusema ni lazima tumpe Mama maua yake.

Nianze kwa simulizi hii inayosema, kuwapo kwa jengo moja katika zahanati ya Mwandet, lililoko Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, likitegemewa kwa huduma zote za kiafya, kulisababisha wakati mgumu kwa watu wengi.

Lakini, adha na usumbufu zaidi ilikuwa ni kinamama wanaojifungua, wagonjwa wa dharura na waliopata ajali.

Uhaba wa madaktari pia ilikuwa changamoto kwa sababu hakuna nyumba za kulala.

Hivyo, wakimaliza kazi waliondoka, lakini hivi sasa wagonjwa wakifikishwa hospitalini, wanakutana na walinzi wanawaamsha madaktari na wanawahudumia.

Ni bashasha kutoka kwa kinamama wanaofurahia kuboreshwa huduma za uzazi na matibabu katika moja ya hospitali jijini Arusha, wanapopongeza kufikiwa na huduma zilizoboreshwa, kutoka awamu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Wakizungumzia miaka mitatu ya Rais, wanaamini kuwa ameokoa wengi, lakini hasa kinamama wanaojifungua pamoja na watoto wadogo.

Wengi, licha ya kuwa ni Watanzania, katika maeneo mbalimbali walijisikia vibaya kuona au kuhisi kuwa serikali haiwaoni kwa sababu ya kukosa huduma za zahanati, elimu na miundombinu, jambo ambalo awamu ya sita inataka kulikomesha.

Maeneo mengi mijini na vijijini yalikuwa hoi, lakini serikali inajitahidi kuondoa shida zao kuanzia umeme, maji na miundombinu.

Tukiangalia huduma za afya ni dhahiri kuwa kulikuwa na changamoto nyingi mno sehemu mbalimbali lakini kinamama wajawazito na watoto ndiyo walioumia zaidi. Ndiyo maana serikali haijamsahau mwanamke.

Pamoja na kumtua ndoo, kumpa nishati safi inaendelea kumbeba kwenye tiba ikiongeza majengo maabara, wodi na vichomea taka.

Vilevile kuna huduma za usafirishaji wa mama na mtoto kwa ajili ya kufikia tiba za rufani. Kinamama na mtoto wamepewa kipaumbele yakijengwa majengo mahususi kwa ajili yao maarufu jengo la mama na mtoto.

Hospitali nyingi zina vyumba vya upasuaji, huduma za maabara zenye ultra sound, x - ray na njia za kutembea zinazowahusisha, pia watu wenye mahitaji maalumu na ulemavu wa viungo.

Ikumbukwe kuwa Tanzania ni kubwa lakini Mama Samia amenyoosha mkono unaofika karibu kila mahali kuwafikishia wananchi maji angalau mita 400 vijijini, wakati mijini ni kila nyumba kufikiwa na maji. Aidha, amewafikishia umeme na barabara pia.

Ni katika kipindi hiki Wizara ya Afya, imeboresha miundombinu ya hospitali mbalimbali pamoja na kuzipandisha hadhi baadhi ya hospitali ili kuziwezesha kutoa huduma bora za afya na kuhudumia wananchi mijini na vijijini kwa weledi.

Kwa ujumla Tanzania imeweka mazingira bora ya utoaji wa huduma za afya kwa mama mjamzito na watoto wachanga, jambo ambalo limechangia kupunguza idadi ya vifo na kuongeza matumaini kuwa kumbe uzazi si kifo.

Kama katika sekta ya afya hakuna kilichosimama tangu Rais Samia, alipoanza kuongoza jahazi. Hospitali zinafanya kazi na huduma za kibobezi zinazidi kuimarishwa.

Kwa ujumla serikali ya Rais Samia inauangalia pia utoaji wa huduma kwa umma, ili usikwamishwe na ulafi wa fedha za umma.

Rais anahimiza kuwa ni lazima kukidhi mahitaji na kutoa huduma ipasavyo na kuonya kuhusu uchepushaji wa fedha za serikali.

Mama anawahimiza viongozi wakati wote, kutumia nafasi walizo nazo kudhibiti wizi wa fedha za umma ambazo ni muhimu kuboresha mazingira ya sekta zote na kubadilisha maisha ya watu kuanzia kwenye miundombinu, afya, ajira na elimu.

Tukiangalia elimu, Tanzania ya leo ina idadi kubwa ya wanafunzi na kila siku Rais anajizatiti kuweka mazingira bora ya kufundisha na kujifunza.

Anaongeza vifaa vya kufundishia, kujenga madarasa ili kupunguza msongamano wa wanafunzi na kuongeza samani.

Sekta ya elimu inahitaji fedha za kutosha ili kuiboresha lakini Awamu ya Sita, imeonyesha utashi wa kisiasa ikijua kuwa elimu inahitaji uwekezaji mkubwa sana na fedha nyingi mno.



# Aweso asimulia chungu, tamu ya Wizara ya Maji

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amebainisha changamoto na mafanikio waliyoyapata kwa kipindi cha miaka minane ya utendaji kazi wake ndani ya wizara hiyo, ikiwamo kuokoa mamilioni ya fedha ambazo zilitakiwa kutolewa kwa makandarasi wanaotekeleza miradi mikubwa ya maji nchini.

Akizungumza juzi katika hafla ya kisekta ya kuadhimisha miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan, Aweso alisema alipoingia wizarani humo bajeti zilikuwa zikikataliwa bungeni na kwamba iko miradi ambayo imejengwa tangu mwaka 1970 na haikuwahi kukamilika.

Alisema bajeti ya maji iliyokuwa ikitolewa siku za nyuma ilikuwa ni ndogo na akiingia kwenye Bunge la Bajeti moja ya changamoto kubwa anayoizungumza ni suala la ufinyu wa bajeti, akieleza kuwa kuna uwekezaji mkubwa unaohitajika, lakini kilichokuwa kikitolewa hakikutumika ipasavyo kwa kuwa alikuwa anakwenda mahali kuzindua mradi, lakini akiondoka anaondoka na maji yake.

"Miaka ya nyuma ilifikia hatua kiongozi anakuja kuzindua mradi kumbe haujakamilika, watu usiku wanaenda kujaza tangi na maboza, nilikaa kwenye wizara, lakini nilikuja nikagundua baadaye kumbe siifahamu, kwenye changamoto ndipo unapopata maarifa. "Wizara ya Maji ni muhimu sana inamhusu masikini na tajiri, unaweza kumpatia maji mwananchi Januari mpaka Desemba, lakini yakikatika tu mchana mtu anasema hivi mama, huyu waziri wa maji bado yuko tu, kazi zetu zinachangamoto nyingi sana, lakini ukiaminiwa, aminika," alisema Aweso.

Aidha, alieleza alivyookoa fedha za miradi kwa kushirikiana na watendaji ndani ya wizara, akibainisha kwamba mradi wa visima vya maji vya Kimbiji, Kigamboni mkoani Dar es Salaam, ulitaka kutekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 700, lakini ulikamilishwa na wahandisi wa ndani kwa bilioni 25, na kufanikiwa kuokoa Sh. bilioni 675.

Kadhalika, ujenzi wa tangi la maji la lita milioni mbili huko Dodoma, mkandarasi alitaka kulijenga kwa Sh. bilioni 2.5 na kwamba alikataa kazi hiyo asipewe mkandarasi badala yake ifanywe na wahandisi wa wizara ambako lilikamilika kwa Sh. milioni 998.

Katika mradi wa Mguru wa Ndege ulitakiwa kujengwa kwa Sh. bilioni 1.2, lakini baada ya maelekezo yake ya kutaka ujenzi utekelezwe na wakandarasi wa ndani hadi kukamilika ulitumia Sh. milioni 550 na kufanikiwa kuokoa karibu asilimia 45.

Alisema walipewa kazi ya kutoa maji ya Ziwa Victoria kuyapeleka Tabora, Igunga mpaka Nzega, mradi wa Sh. bilioni 600, na hadi kukamilika waliokoa Sh. bilioni 30, ambazo zilitumika kufikisha huduma hiyo Tinde na Shelui.

"Sio rahisi, tunafanya kazi ya hatari ambayo unapambana na mambo mengi, lakini Rais ametusimamia, Mkuu wa Chuo cha Maji, tulimweleza kwamba wizara haiwezi kwenda bila kuwa na watumishi kwasababu moja ya changamoto kubwa pia ilikuwa ni uhaba wa watumishi, nikasema lazima tukifufue chuo chetu kizalishe watumishi na kufanya utafiti unaoendana na changamoto za wizara," alisema Aweso.

Hata hivyo, alisema mradi wa Kiaka Bunazi ulitakiwa kujengwa kwa Sh. bilioni 20, lakini alikataa na kuelekeza utekelezwe na wakandarasi wa ndani ya wizara ambao waliukamilisha kwa Sh. bilioni 15.7 akieleza kuwa huko ndiko wizara hiyo ilikotoka.

"Tumeingia kwenye hii wizara ilikuwa ni ya kero na lawama tu, tuliwahi kwenda eneo linaitwa Mwakitolio, Shinyanga Vijijini, kiongozi unafika wananchi wanakupokea na ndoo za maji, ukimuuliza mhusika wa pale hapa mbona hela imetolewa Sh. bilioni 1.2 kwanini watu hawapati maji, ananiambia waziri naomba nikunong'oneze.

"Nikamwambia hapana kwanini watu hawapati maji anasema waziri sijawahi kuona wananchi wachawi kama kijiji hichi, mabomba yanapaa usiku. Tukaenda Handeni unamuuliza mkandarasi nionyeshe bwawa, Sh. milioni 600 imeenda bwawa halipo kibanda kile anakuambia milioni saba, kuna kusoma na kuelimika, wasomi tutumie taaluma zetu kuwasaidia watanzania waliotupa dhamana," alikumbusha.

Waziri Aweso, alisema baada ya kujifungia katika kikao na watumishi wa wizara hiyo walisemana na kuambiana ukweli, huku wakiwekeana utaratibu wa ulazima wa kufanya 'engineering estimation' akimaanisha makadirio ya uhandisi kabla ya utekelezaji wa mradi.

"Kila mmoja akijituma tukaweka lengo kwamba zikitajwa wizara tatu ya kwetu lazima iwe namba moja, haikuwa rahisi, tulikuwa na miradi 177 ambayo imetolewa fedha, lakini haitoi maji, leo yote tayari tumeshaikwamua," alisisitiza Aweso.




# Kongamano la mawasiliano kuwaleta wanazuoni 300

**Na Enock Charles**

ZAIDI ya wanazuoni 300 wakiwamo wanataaluma, watafiti, wahariri, wamiliki wa vyombo vya habari na maofisa wa serikali wanatarajiwa kushiriki Kongamano la 14 la wanazuoni la Mawasiliano Afrika Mashariki (EACA) litakalofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) mwezi Agosti, mwaka huu.

Kongamano hilo linalotarajiwa kufanyika kwa siku tatu kuanzia Agosti 28 linatarajiwa pia kuwa na washiriki kutoka mataifa zaidi ya 10 duniani waliothibitisha ushiriki wao wakiwamo kutoka Marekani, China, Uingereza, Norway na Afrika Kusini.

Akizungumza na vyombo vya habari, jijini Dar es Salaam juzi, Amidi wa Shule ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (SJMC), Dk. Mona Mwakalinga, alisema kongamano hilo linatarajiwa kuitangaza lugha ya Kiswahili duniani pamoja utalii wa Tanzania duniani.

Alisema matarajio yao kongamano hilo litapanua mitandao ya kitaaluma, kupata elimu na maarifa mapya ambayo yataharakisha maendeleo katika taaluma ya habari na mawasiliano kwa kubadilishana taarifa za kiutendaji ndani ya vyombo vya habari.

"Washiriki watapata fursa ya kubadilisha taarifa na maarifa katika vyombo vya habari ndani na nje ya nchi au ndani ya idara za mawasiliano kwenye taasisi za serikali na zile za binafsi au utafiti ambao umefanyika katika sekta hii ya habari," alisema Dk. Mona.

Kuhusu kukikuza kiswahili kama mojawapo ya lugha kuu za mawasiliano barani Afrika, Mhadhiri wa UDSM, Dk. Egbert Mkoko alisema, itakuwa mojawapo ya mada katika kongamano hilo ili kuhakikisha Afrika inakuwa na lugha zake za mawasiliano badala ya kuendelea kutegemea lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kifaransa.

"Kumekuwa na mjadala kwa muda mrefu sisi kama Afrika kuwa na lugha yetu ya mawasiliano na sote tunajua kwamba lugha rasmi ambazo zinatumika katika mataifa mengi nyingi zimetoka huko Ulaya, Kireno, Kiingereza, Kifaransa ukiondoa Kiarabu tu ambacho kimetoka barani Asia, lakini nyingi zimetoka Ulaya," alisema Dk. Mkoko.

"Sasa sisi kama Afrika tuna nini cha kujivunia kuhusu lugha ya mawasiliano, Kiswahili kimekua na kimesambaa sasa tunataka tujadili namna gani kinaweza kikachukuliwa kama lugha kuu ya mawasiliano kwa sisi Waafrika," alisema Dk. Mkoko.

Kuhusu utalii, alisema itakuwapo mada kuhusu ushiriki wa waandishi wa habari katika utalii akisema upo muhimu mkubwa kwa waandishi wa habari kushiriki kukuza utalii kwa maendeleo ya nchi na nchi nyingine za Afrika akitolea mfano wa Filamu ya Royal Tour ambayo inahusu utalii wa Tanzania iliyofanywa na Rais Dk. Samia Suluhu na jinsi vyombo vya habari vilivyoshiriki kuitangaza duniani.

Mada nyingine alisema ni kuhusu hatma ya habari za kiuchunguzi ambazo kwa sasa zimeadimika sio Tanzania pekee bali pia katika maeneo mengine barani Afrika na namna ya kurejesha mvuto wa habari hizo.

Kongamano hilo la 14 ni la pili kufanyika nchini baada ya la kwanza kufanyika katika Chuo cha Mtakatifu Augustine jijini Mwanza mwaka 2013, Dk. Mkoko alisema mada zitakazojadiliwa ni pamoja na 'Afrika na Mjadala wa Kimataifa Kuhusu Mawasiliano na Vyombo vya Habari' ikiwa ndiyo mada kuu zikiwamo na mada zingine ndogo 12.

# Mahakama yatupa ombi mtumishi JWTZ kufutiwa kesi

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imetupilia mbali ombi la upande wa utetezi la kutaka aliyekuwa mtumishi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Sufian Kideku na wenzake wanaotuhumiwa kwa kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha wafutiwe mashtaka yao, baada ya upande wa mashtaka kutokuwa na mashahidi.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mfanyabiashara Selestine Kamuli, mkazi wa Kizuka Morogoro na Husein Mwinyijuma, mkazi wa Gairo, Morogoro ambaye ni mtumishi wa JWTZ.

Uamuzi huo ulitolewa na Hakimu Mkazi Mkuu, Aaron Lyamuya wa mahakama hiyo baada ya upande wa utetezi kuwasilisha ombi mahakama ifute kesi hiyo na kuwaachia huru washtakiwa kutokana na upande wa mashtaka kushindwa kuleta mashahidi mahakamani.

"Upande wa mashtaka kuomba ahirisho haikumaanisha kwamba wanatumia mamlaka yao vibaya, hawakuwa na kosa katika ombi hilo, kwa hiyo mahakama inatupilia mbali pingamizi hili," alisema Hakimu Lyamuya.

Hata hivyo, Hakimu Lyamuya ameutaka upande wa mashtaka kuleta mashahidi tarehe ijayo na wasipowaleta anaifuta kesi hiyo. Kesi imeahirishwa hadi Machi 28, mwaka huu.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka manne ambayo ni unyang'anyi wa kutumia silaha, kujifanya mtumishi, kuteka na kujaribu kutishia kwa lengo la kujipata kitu, wanayodaiwa kutenda Mei 17, 2023 eneo la Zaramo mtaa wa Jamhuri Posta, Ilala, Dar es Salaam.


MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA

Salamu za Pongezi

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa **Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)** Tunakupongeza kwa utendaji na uwajibikaji wako katika kusimamia na kutekeleza yale uliyoyaahidi ndani ya kipindi hiki cha Miaka Mitatu.

***Tunakuombea afya njema na tuko pamoja katika kuhakikisha agenda ya maendeleo ya Watanzania inafanikiwa.***



MH. Dkt. SAMIA SULUHU HASSAN
RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

*TPA The Gatway to Global Trade and Prosperty*

P.O.BOX 9184 Dar es Salaam One Bandari Road, Kurasini, Tanzania
+255 22 2110401/5; +255 22 2110371/5; +255 22 2137631/2
Namba za Simu bure: 0800 110032, 0800110047, http://www.ports.go.tz

tanzaniaportshq tanzaniaportshq TPAHQ tanzaniaportshq



## RC azuia uhamisho walimu, awapa maagizo wakurugenzi

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, amezuia uhamisho wa walimu wa msingi na sekondari kufanyika katika wilaya zote mkoani kwake.

Pia amewaagiza wakurugenzi wa halmashauri kuwahamisha mjini walimu walioko kwenye shule zenye idadi kubwa ya walimu, kupelekwa shule za vijijini na pembezoni, ambazo zinakabiliwa na upungufu wa walimu.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki, wakati akifungua kikao cha kamati ya ushauri cha mkoa huo.

"Nataka kuwepo na msawazo wa walimu, maana kada hii inakuwa na uhamisho mwingi mno. Wanajifanya kuwa na matatizo ya kiafya," alisema Sendiga.

Aidha, alisema watumishi wa umma wanapaswa kufanya kazi mahali popote, ila walimu na wauguzi wana haki ya kukaa popote ili wawahudumie wananchi inavyotakiwa.

Katika hatua nyingine, Katibu Tawala Msaidizi, Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara, anayeshughulikia Uratibu na Mipango, Lusungu Mwilongo, aliwasilisha Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Mwaka mpya wa fedha 2024/25, ambayo Manyara itatumia Sh. bilioni 278.8

Mwilongo, alisema vipaumbele vyao vitakuwa ni amani na utulivu, kuboresha huduma za kijamii, ukamilishaji wa miradi viporo, ukusanyaji wa mapato na uchaguzi wa serikali za mitaa.

Wakati huo huo, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Babati (BAWASA), ikipanga kutumia Sh. bilioni 25 kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 80 hadi asilimia 95.

Alisema Wakala wa Maji na Usambazaji wa Maji Vijijini (RUWASA), imepanga kutumia Sh. bilioni 15.8, ambapo watatekeleza miradi 36 inayoendelea na miradi miwili mipya.

# Mratibu Elimu ashangaa watuhumiwa ubakaji wanafunzi kutokamatwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MRATIBU wa Elimu wa Kata ya Daraja Mbili jijini Arusha, Fausta Njau, ameeleza kushangazwa na mamlaka za kisheria kuwafumbia macho baadhi ya watuhumiwa wa ukatili wa kingono dhidi ya wanafunzi.

Amesema vitendo vya ulawiti na ubakaji kwa wanafunzi wa kata hiyo vimekithiri, ikiwamo wazazi kutuhumiwa kwa makosa hayo.

Akiwasilisha taarifa hiyo mwishoni mwa wiki, mbele ya Sekretarieti ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), wilayani humo, Njau, alisema hali hiyo imemfanya achukue hatua za kuwahamishia baadhi ya watoto kwenye vituo vya kulea watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Sekretarieti hiyo ilikuwa ikiongozwa na Katibu wa CCM, Wilaya ya Arusha, Timoth Sanga.

Kutokana na kushamiri kwa matukio hayo, Mratibu huyo aliiomba serikali kuongeza nguvu katika kata hiyo, kwa kuchukua hatua za kisheria, dhidi ya watuhumiwa wanaohusika, kwa kuwa baadhi yao wakifikishwa polisi wanarudi mtaani.

"Ni kweli kama wananchi walivyolalamika hapa katika kata hii, kuna changamoto kubwa ya wazazi kubaka na kulawiti watoto wao, ambao ni wanafunzi katika shule zetu za msingi na wanakamatwa na kupelekwa polisi, lakini baada ya muda tunawaona mtaani," alisema.

Kwa mujibu wa mratibu huyo, yuko mkazi wa kata hiyo aliyedhibitiwa, ambaye ni baba mzazi aliyekuwa akitaka kuwafanyia vitendo hivyo watoto wake wawili wa kuwazaa.

Kutokana na tishio hilo la ukatili, Mratibu huyo alidai amelazimika kuwachukua watoto hao na kuwahamishia kwenye kituo cha makazi ya watoto cha Amani.

"Lakini tuna mzazi mwingine aliyefahamika kwa jina la Hashim Ngude ambaye alimbaka mtoto wake wa darasa la tano, mwenye umri wa miaka tisa na kufumaniwa na wananchi, huyu tulimkamata na kumpeleka kituo cha polisi, ila yupo mtaani hata hatujuwi ni kwa sababu gani ametoka.

"Huyo mwanafunzi pia tumemwamishia Kituo cha Amani. Matukio ni mengi ya ubakaji lakini mwaka jana kesi tano za watoto waliobakwa na wazazi zilipelekwa mahakamani na zipo katika hatua mbalimbali," alisema.

Kutokana na malalamiko hayo ya wananchi, Katibu wa CCM wa Wilaya ya Arusha, Sanga, aliwasiliana na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Arusha, George Malima, ambaye hata hivyo alikiri kuifahamu kesi hiyo.

Katika majibu yake, Mkuu huyo wa Polisi, alisema tayari jalada la kesi ya mkazi huyo, limepelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS) kwa hatua zaidi.

Baada ya majibu hayo, pia Sanga aliahidi kuwasiliana na Mkuu wa Dawati la Jinsia la Polisi ili kujua hatua zaidi zilizochukuliwa kuhusiana na matukio hayo.

Katika hatua nyingine, Sanga alimwagiza Diwani wa Kata ya Daraja Mbili, Prosper Msofe, kuhakikisha kuwa wanadhibiti tabia ya baadhi ya wananchi wa kata hiyo, kunywa pombe haramu hasa asubuhi na kulewa badala ya kufanya kazi, hali inayosababisha kufanya vitendo ambavyo havina maadili mema kwa jamii.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Daraja Mbili, Anzamen Sawe, alisema kuanzia sasa mwananchi atakayekutwa amelewa asubuhi atakamatwa, ikiwa ni pamoja na wauzaji wote wa pombe haramu na wanaofungua baa muda wa kazi.



Mkuu wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Kasilda Mgeni (kushoto), akikabidhi msaada wa taulo za kike kwa mwanafunzi wa kidato cha tatu, Mariam Said, kwa niaba ya wanafunzi wenzake wa Shule za Sekondari za Migharen na Kwakoko, wilayani humo jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Serikali yamaliza mgogoro wa ardhi wa miaka 17

**Novatus Makunga,** ARUSHA

SERIKALI mkoani Arusha, imemaliza mgogoro wa muda mrefu wa umiliki wa viwanja namba 624 na 625 vilivyoko Kitalu F, eneo la Njiro jijini Arusha, kati ya ndugu wawili wa familia moja na mfanyabiashara aliyetajwa kwa jina moja la Jeina.

Mgogoro huo uliochukua miaka 17, unatokana na maofisa ardhi wa Jiji hilo kugawa viwanja hivyo mara mbili, kwa watu tofauti.

Juzi, baada ya kutatua mgogoro huo, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, amemwagiza Ofisa Ardhi wa Wilaya hiyo na Kamishna Msaidizi wa Ardhi mkoani hapa, kuandaa hatimiliki ndani ya siku saba ili kutoa haki kwa mmiliki halali.

Mongella, alitatua mgogoro huo baada ya kuzungumza na kwenda eneo la viwanja hivyo na walalamikaji, Anasia Malewas na Jonas Malewas, ambao walalamikia idara ya ardhi, kugawia viwanja vyao kwa mtu mwingine anayetajwa kwa jina la Jeina.

Baada ya majadiliano ya kina, kutoka pande zote Mongella, amemwagiza Kamishna Msaidizi wa Ardhi wa Mkoa wa Arusha, kuandaa hati za watu wote watatu kwa kutumia 'hatimiliki' iliyopo na kurekebisha ukubwa wa viwanja ili wote watatu wapate hati mpya kwa kila mmoja.

"Kwa kuwa hati miliki na alama za mipaka zipo, nawapa wiki moja kufanya zoezi hili, kurekebisha ukubwa wa eneo na kuandaa hati nyingine, kila mmoja apate hati mpya," alisema Mongella.

Kiwanja kimoja kitakuwa na mita za mraba 588, cha pili 740 na cha tatu kitabaki na mita za mraba 440 na kila mmoja akipewa hati mpya atarudisha hati halisi.

Hata hivyo, walalamikaji wote wameridhika na maamuzi hayo na kukubali kupewa hati mpya.

Mlalamikaji wa kwanza, Anasia Malewas, alimshukuru Mongela, kwa kufanya uamuzi wa busara ambayo yamewawezesha kupata haki na siyo kupata haki pekee bali kila mmoja kupata eneo ambalo wamekuwa wakihangaikia kwa muda mrefu.


"Mimi binafsi namshukuru Mongela, Mungu ambariki, naamini sote tutapata haki yetu, ambayo tunahangaika nayo kwa miaka 17 sasa, Mungu ambariki sana," alisema Anasia.

Lembris Kipuyo, ambaye amejitambulisha kuwa ni mtetezi na mwakilishi wa walalamikaji, ambao alieleza kuwa wote ni wajane, alimshukuru Mongela, kwa uamuzi huo.

Alisema maamuzi hayo yanaenda kuwasaidia kina mama wajane hao waliokuwa na hati miliki ambazo wamekuwa wakilipa kodi zote lakini viwanja vyao vimekuwa na mkanganyiko wa kitaalamu.

"Migogoro haijengi, bali inaumiza mioyo ya watu na kusababisha chuki miongoni mwa wanajamii, ni bora iepukwe," alisema Kipuyo ambaye ni Mkuu wa Wilaya mstaafu.

Hata hivyo, Kamishna Msaidizi wa Ardhi wa Mkoa wa Arusha, Geoffrey Mwamsojo, aliahidi kutekeleza agizo hilo ndani ya siku saba.





# Wananchi 'wamkaba' mwenyekiti arejeshe makusanyo ya fedha

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Kata ya Kagongwa Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamemkaba koo mwenyekiti wao, Michael Shija wakimtaka arejeshe shilingi milioni saba zilikusanywa kwa ajili ya kununua eneo la mazishi.

Mwenyekiti huyo anadaiwa kuzibadilisha matumizi fedha hizo pasipo kufanyika kwa vikao na kuamua kujenga matundu ya vyoo 10 katika Shule ya Msingi Kanegere.

Hivyo, walimtaka kurejesha fedha hizo juzi wakati wa mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba, uliokuwa na dhumuni la kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Wakiwa katika mkutano huo wananchi hao walidai kuwa ni kawaida kwa mwenyekiti huyo kukusanya michango na kutosoma mapato na matumizi.

Mmoja wa wananchi hao, Justini Mabula alisema, mwaka jana walichangisha fedha za kununua eneo la maziko na zilifika Sh.milioni saba, mpaka sasa hazijulikani zilipo na hakuna eneo lililonunuliwa.

Alisema wanapohoji hawapewi majibu ya kuridhisha kutoka kwa viongozi.

Ofisa Tarafa ya Isagehe, Vicent Ndesekio alisema, fedha zote zinazotolewa na wananchi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo zinatakiwa kupitia kwenye akaunti ya kijiji, mtaa au kata husika, ndipo zianze kutumika kwa lengo lililokusudiwa.

Alisema kwa kitendo alichokifanya mwenyekiti huyo ni kosa kisheria.

Alisema endapo zilibadilishiwa matumizi alitakiwa kuitisha tena mkutano na kueleza hoja zake na wananchi waridhie tofauti na alivyofanya, hivyo kungana na wananchi kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa kabla hajachukuliwa sheria za kinidhamu.

Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba alisema kutowasomea wananchi mapato na matumizi na kubadilisha fedha za maendeleo pasipokuwa na vikao vya maamuzi ni kwenda kinyume na kunasababisha kuibuka kwa malalamiko na migogoro isiyokuwa na tija.

Alisema ili iwe fundisho kwa wenyeviti wengine ni vema fedha hizo zikarejeshwa na sio vinginevyo.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, alisema kama mwenyekiti huyo asiporejesha fedha hizo basi vyombo vya sheria vimshikilie na kumfikisha mahakamani kujibu tuhuma za wizi wa fedha za umma.

Alisema viongozi wenye tabia za namna hiyo wamekuwa wakikichafua chama pamoja na serikali.

Mwenyekiti huyo alikiri kupokea fedha hizo kutoka kwa wananchi kwa ajili ya ununuzi wa eneo la maziko na mpaka sasa hajanunua kwa sababu alizibadilishia matumizi na kwenda kujenga matundu 10 ya vyoo katika Shule ya Msingi Kanegere.

Aidha aliahidi kurejesha fedha hizo, huku akianza kwa kurejesha Sh.milioni nne kati ya milioni saba zilizokuwa zimetolewa na wananchi.

Hivyo aliomba kupewa muda ili kutafuta kiasi kilichobakia huku akiwataka kutomchukulia tofauti kwani alikuwa anatatua tatizo la ukosefu wa vyoo shuleni.




Waziri wa Madini, Antony Mavunde, akizungumza na wananchi na wafanyakazi wa Kampuni ya Barrick katika hafla ya uzinduzi wa kituo cha mafunzo cha Barrick kilichojengwa ndani ya mgodi wa Buzwagi uliopo Kata ya Mwendakulima Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Kamati ya Bunge yaitaka TTCL kujiendesha kibiashara

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KUFUATIA uwekezaji unaoendelea katika Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) ukiwamo ujenzi wa Mkonga wa Taifa, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imelitaka shirika hilo kujiendesha kibiashara.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Seleman Kakoso, aliyasema hayo juzi na kueleza kuwa kupitia mkonga huo TTCL litaingiza fedha nyingi za ndani na nje ya nchi, hivyo ni wakati sasa umefika wa shirika hilo kujiendesha kibiashara.

Aidha, aliitaka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuwa wabunifu pamoja na kuja na mawazo ya nchi iwe na 'satelite' yake yenyewe ili kuimarisha mfumo wa teknolojia.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema ujenzi wa Mkonga wa Taifa upo katika wakati wake ambapo kwa sasa dunia inakwenda kwenye uchumi wa kidigitali.

Mtendaji Mkuu wa TTCL, Peter Ulanga akisoma taarifa ya ujenzi wa mkonga huo, alisema mwaka wa fedha 2023/2024 wizara hiyo ilitengewa Sh.bilioni 80 kwa ajili ya ujenzi wa kilomita 1,600 na vituo 32 vya Mkonga wa Taifa pamoja na kufanya upanuzi wa njia za usafirishaji wa mawasiliano kutoka 800 Gbps kwenda 2000 Gbps.

Alisema pia wanafanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa vituo vya kutunzia taarifa Zanzibar na Dodoma na kuunganisha taasisi 50 kwenye Mkonga wa Taifa, pamoja na kuunganisha nchi ya Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC).

"Awamu ya kwanza ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa ilianza mwaka 2009 ikiwa na uwezo wa 40G na baadaye kuongezwa uwezo kuwa 200G hadi 400G kwa Singida, Shinyanga na Mwanza," alisema Ulanga.

# Ukifichua wanaoiba miundombinu TANESCO donge nono litakuhusu

**Na Benny Kingson,** TABORA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Tabora limewaonya watu wanaohujumu miundombinu ya umeme, huku likiahidi kutoa donge nono kwa watakaofanikisha kutoa taarifa na kukamatwa wahusika.

Kaimu Meneja wa TANESCO Mkoa wa Tabora, Seleman Ng'anzi, alitoa onyo na dau hilo wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake juu ya hali ya ukosefu wa umeme katika baadhi ya maeneo.

Pamoja na mambo mengine alitaja kuwapo kwa hujuma za mara kwa mara zinazopunguza ufanisi katika kazi zao za usambazaji umeme.

Aidha alikemea tabia hizo za wizi wa miundombinu mbalimbali ikiwamo pia tabia za wananchi kupanda miti na mazao ya kudumu katika maeneo ya chini zinapopita nyaya za umeme na baadaye kusababisha uharibifu wa nyaya hizo.

Ng'anzi alisema watakaosaidia kutoa taarifa za wanaoiba umeme kwa kujiunganishia na kufanikisha kukamatwa kwa wahusika watalipwa Sh.100,000 na zaidi huku watuhumiwa wakilipishwa faini.

"Watakaotoa taarifa za watu wanaoiba mafuta ya transfoma, wizi wa nyaya za umeme, nguzo, kuchoma nyaya hizo na nguzo zetu na tukafanikiwa kuwakamata tutalipa kuanzia Sh.500,000 na kuendelea kulingana na ukubwa wa tukio na bajeti yetu kwa kipindi husika," alisema Ng'anzi.

Aidha alisema kumekuwapo na tabia ya watu kupanda miti sehemu zilipopita nyaya za umeme na kuiacha ikue bila kuipunguzia matawi, akisema hatua hiyo ni hatari kwa maisha yao na mali zao hivyo kuwataka waache suala hilo.

Alisema vitu hivyo vimekuwa vikikwamishwa shughuli za utoaji huduma bora kwa wateja na kusababisha umeme kukatika ovyo.

Ng'anzi alihimiza jamii kuendelea kuilinda miundombinu ya umeme na kutoa taarifa haraka kwenye ofisi zao pindi wanapoona inahujumiwa ili iwasaidie na kuokoa gharama zitazosababishwa na hasara zitokeazo.

Alisema kero ya kukosekana kwa huduma ya kutosha ya umeme katika wilaya za Urambo na Kaliua itamalizika hivi karibuni kufuatia ujenzi wa vituo vya kupozea umeme vinavyojengwa kwenye wilaya hizo.

Awali baadhi ya wakazi wa wilaya hizo walioomba serikali kuongeza juhudi katika kukabiliana na tatizo la upatikanaji umeme ili kurahisisha shughuli zao za kiuchumi na kijamii.

Nipashe

# MIAKA 3
## AWAMU YA SITA

Jumanne Machi 19, 2024





Ukurasa 12

Diplomasia, ushirikiano kimataifa Vatican kusaidia kuibua teknolojia



Ukurasa 13

Mama alivyokomesha jinamizi la uzazi kuwa sababu ya vifo vya wajawazito

# Wadau wampa '5' ustahimilivu kisiasa ustawishaji, kusuka demokrasia upya



Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Rais Samia Suluhu Hassan, akikagua gwaride la heshima. **PICHA: IKULU**

WAKATI Rais Samia Suluhu Hassan, akitimiza miaka mitatu madarakani leo, wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanamuona kama kinara wa kujenga ustahamilivu mkubwa wa kisiasa.

Wanagusia kauli zake akisema 'siasa siyo uadui mikutano ya hadhara ni rukhsa na pia 'sina kundi, wakieleza kuwa zimedhihirisha R4 anazozisimamia ambazo ni reconciliation kwa maana ya maridhiano, resilience ambao ni ustahamilivu na reforms akimaanisha mabadiliko na rebuilding au kujenga upya.

Ni mwaka mmoja na miezi miwili na nusu, tangu Rais Samia atoe rukhsa ya mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa na matunda ya kauli hiyo yameonekana.

Katika kipindi hicho ambacho tumeshuhudia mikutano na maandamano hususani ya CHADEMA, ambayo yamefanyika katika majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Arusha; yaliyohitimishwa kwa mikutano wa hadhara na hoja mbalimbali zinazogusa wananchi.

Washiriki wa maandamano hayo wanabeba mabango yenye jumbe mbalimbali ikiwamo madai ya katiba mpya, marekebisho ya sheria za uchaguzi na kukabili mfumuko wa bei ili kupunguza gharama za maisha.

Hatua ya wananchi kuandamana kwa amani tena wakilindwa na polisi bila kupigwa mabomu ya machozi, ni matunda ya ustahamilivu wa Rais Samia kukubali kusikiliza wale wanaomkosoa.

Kupitia R4, Watanzania wameendelea kuimarisha utu, umoja, udugu, maelewano, ushirikiano, pamoja na amani, ndivyo wachambuzi wanavyosema.

Baada ya mikutano ya hadhara kwenye majiji manne, CHADEMA ilitoka na Azimio la Mtwara lenye hoja 10 wanazotaka zifanyiwe kazi kuboresha mfumo wa uchaguzi nchini na awamu ya maandamano ambayo yamepangwa kufanyika katika kila makao makuu ya mikoa yote nchi nzima kuanzia Aprili 22 hadi 30 mwaka huu.

Akitoa maazimio hayo kwa niaba ya Kamati Kuu ya chama hicho mapema mwezi huu, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, anasema kupatikana katiba mpya ni miongoni mwa mambo wanayoendelea kusisitiza.

Katiba mpya, tume huru ya uchaguzi na kubadilishwa mfumo mzima wa kusimamia na kuendesha uchaguzi mkuu na uchaguzi wa serikali za mitaa, ni suala la msisitizo analosema Mbowe.

Mchambuzi mmoja ambaye hakupenda atajwe jina lake, anasema maridhiano na ustahamilivu ni msingi katika kupata maendeleo hasa watu wanapokuwa na uhuru wa fikra.

### MSIMAMO WA RAIS

Alipokuwa akitangaza rukhsa ya mikutano Januari 3, 2023, anasema ni haki ya kikatiba kwa vyama kufanya mikutano ya hadhara na kukumbusha siasa za kistaarabu za kuijenga nchi.

"CCM tunaamini kukoselewa na kukosoa, kosoeni, mimi naamini mkinikosoa najua changamoto iko hapa na niikifanyia kazi na kuitatua basi nitaendelea kuwepo. Ndio maana siwaiti vyama vya upinzani bali ni vyama vinavyotuonesha kasoro."

"Kazi yetu itakuwa ni kutekeleza. Twendeni tukafanye siasa, kama tumekosea haki za binadamu tuambieni,lakini tukitukanana, tukaanza kurusha kashfa nchi haitakalika. Niwaombe ndugu zangu twendeni tufanye siasa, isemeni serikali na ikosoeni. Ukiamua kupanda jukwaani jizatiti na pale ambapo tumefanya vizuri semeni."

Anaongeza kuwa anafahamu watakwenda kusema serikali ina madeni lakini waseme madeni yamefanya nini? Yanajenga SGR hadi Kigoma.

Akaongeza kuwa uongo haujengi, bali wajenge hoja, na kuwahakikishia kuwa amezungumza na vyombo vya ulinzi na usalama na vitawalinda.

Katika hatua nyingine Rais Samia, wiki iliyopita anaweza wazi msimamo wake kichama na kiserikali, akiwaambia Watanzania na wana-CCM kuwa hana kundi na kusema 'mimi ni mtu wa wote'.

"Mkijitizama humo, makundi mnayoyajua wote mmo humo ndani, ninachotaka mimi Watanzania kwa pamoja tufanye kazi, tusogeze nchi yetu mbele, sina kundi.

"Sasa wale wanahoji kujitambulisha huyu ni wa mama huyu siyo wa mama, mimi mama nina watoto wote, wote wangu ninalea. Anayefanya vizuri wangu, anayefanya vibaya wangu, mwingine nitampa zawadi na mwingine nitamchapa mikwaju.

"Na wapo ninawachapa, ninawaweka nje, akishapata adabu yake ninamwambia njoo tufanye kazi. Kama makundi yenu huko, mimi hayanihusu, ninataka tufanye kazi 2024 na 2025 tuvuke vizuri," anasema.

### KAULI YA CCT

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Mchungaji Moses Matonya, anampa 'tano' Rais Samia, kwa kuonesha ujasiri wa kuifungua nchi kiuchumi, kisiasa na kidiplomasia, akisema 'ni jasiri na amethubutu'.

Mchungaji Matonya anayasema hayo anapozungumza na Nipashe kuhusu miaka mitatu ya Rais Samia madarakani.

Anasema utendaji wake umeleta mageuzi na matumaini ya kiuchumi na kisiasa kwa Watanzania, hivyo kuimarisha demokrasia na ustawi wa wananchi.

"Anachukua uongozi wakati wa janga la COVID-19 na uchumi ukiwa umeshuka sana, yalikuwa mazingira magumu. Mataifa mengi yalikuwa zimeathiriwa," anaeleza

Anaeleza kuwa amekuta pia miradi mikubwa ya kiuchumi na kulikuwa na changamoto ya ni wapi pa kupata fedha katika uchumi uliodorora. Bado aliyachukua yote na kuyafanyia kazi.

INAENDELEA UK.14

# Diplomasia, ushirikiano kimataifa Vatican kusaidia kuibua teknolojia

## • Tanzania kuwa ukanda viwanda Afrika

**NA ELIZABETH ZAYA**

WATANZANIA kutoka Arusha hadi Zanzibar, leo wanakiangalia kishindo cha awamu ya sita, wakati Rais Samia Suluhu Hassan, akitimiza miaka mitatu ya kuliongoza taifa, jukumu alilolianza Machi 19, 2021.

Kama ambavyo ni desturi kwa kila kiongozi kuwa na vipaumbele anapoingia madarakani, jambo muhimu kwa Rais ni kuimarisha mahusiano ya kimataifa na kidiplomasia.

Ni kazi anayoianza miezi miwili baada ya kuapishwa, akiitembelea Kenya Mei 2021, kufuatia mwaliko wa Uhuru Kenyatta aliyekuwa rais kipindi hicho.

Wakati huo, Kenya na Tanzania zilikuwa zikipishana kwenye masuala ya kibiashara na uwekezaji na alitumia ziara hiyo kusawazisha.

Rais Samia, akiwa na ratiba iliyomfikisha sehemu mbalimbali na pia kuhutubia Bunge la Seneti, anawahakikishia kuwa amefika kuleta suluhu ikiwamo kuondoa baadhi ya vikwazo vya kibiashara na kiushirikiano ambavyo mataifa hayo wanachama waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), walikuwa wakipishana.

Mbali na Kenya, Rais Samia anawatembelea wanachama wa nchi nyingine za Afrika ya Mashariki kama Uganda na Rwanda, kadhalika ukanda wa Ushirikiano wa Maendeleo wa Kusini mwa Afrika (SADC), akizuru Zambia, Namibia na Malawi.

Katika jukumu hilo amelenga kuimarisha uhusiano wa kimataifa na kidplomasia hususani katika uchumi kwa kuboresha mazingira ya kibiashara, kuhamasisha uwekezaji na mtangamano wa Afrika.

Katika nchi nyingi ambazo Rais Samia amekuwa akifanya ziara, mbali na kuhamasisha uwekezaji, amekuwa akisaini mikataba au hati za makubaliano zenye lengo la kuanzisha ushirikiano katika maeneo ya uwekezaji kama kwenye viwanda, biashara, afya, elimu, teknolojia, maji na kilimo.

Juhudi hiyo ya kuimarisha uhusiano huo, ameivusha katika mataifa mbalimbali yaliyo nje ya Afrika Mashariki na baadhi yake ikiwa ni Indonesia, Norway, Saudi Arabia, India, Mataifa ya Falme za Kiarabu, Misri, Ethiopia, Vatican, Marekani na China.

Hivi karibuni wakizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, viongozi ambao wamekuwa wakiambatana na Rais katika safari hizo za kuimarisha uhusiano wa kimataifa, na kutafuta fursa mbalimbali kuboresha diplomasia ya uchumi, wanaeleza faida zilizopatikana kwenye ushirikiano huo wa kimataifa.



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa na Papa Francis nchini Vatican hivi karibuni. **PICHA: RADIO VATICAN**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, anasema mafanikio ni mengi akitaja kuongezeka idadi ya wawekezaji bila kusahau ajira kwa makundi mbalimbali.

Anafafanua kwamba katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba mwaka 2022 Tanzania ilivutia uwekezaji wa mitaji ya Dola za Kimarekani milioni 770 na kipindi kama hicho mwaka jana iliongezeka kufikia mitaji ya Dola za Kimarekani milioni 1,396.

Miradi iliyosainiwa, kuanzia Oktoba hadi Desemba mwaka 2022 ilikuwa 58 lakini iliongezeka hadi kufikia 213, kipindi kama hicho mwaka jana, anasema Profesa Mkumbo.

Katika eneo la ajira, kuanzia Oktoba hadi Desemba 2023 Watanzania 14,390 waliajiriwa ikilinganishwa na 10,216 waliopata ajira mwaka 2022 kuanzia Oktoba hadi Desemba.

"Mfano ziara ya China, imeleta wawekezaji katika sekta ya viwanda vikubwa, kikiwamo cha kutengeneza vioo vya ujenzi ambacho ni cha nne kwa ukubwa barani Afrika kilichopo Mkuranga mkoani Pwani," kwa mujibu wa Waziri.

Anafafanua zaidi kuwa China imeendelea kuwa na uwekezaji mkubwa ikijenga ukanda wa viwanda wa Sino-Tan Induatrial Park, karibu na bandari kavu ya Kwala iliyoko Vigwaza mkoa wa Pwani.

Anasema uwekezaji wa Sino-Tan Industrial Park ni wa Dola za Kimarekani utakapokamilika utakuwa na thamani ya Dola za Kimarekani bilioni tatu zaidi ya Shilingi trilioni 11.

Ziara ya Misri nayo imesaidia kuanzisha kiwanda cha kuzalisha transfoma, nyaya na vifaa vingine vya umeme, ambacho kipo Kibaha mkoani Pwani.

Anataja mafanikio ya ziara ya Indonesia, kwamba nayo imeleta kiwanda cha mbolea mkoani Mtwara kitakachozalisha bidhaa hiyo kwa kutumia gesi asilia na pia kuongeza viwanda vya sukari.

"Ziara ya India inakwenda kuzaa matunda kwa kuwa inatarajia kuleta wawekezaji katika eneo la viwanda vya kuunganisha matrekta kwa ajili ya kilimo." Anasema Waziri Mkumbo.

Ziara nyingine ni ya Vatican ambako Rais Samia alikwenda baada ya mwaliko wa Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani Papa Francis pamoja na viongozi wengine, Tanzania itanufaika na uhamilishaji wa teknolojia ili kuiboresha na kuifanya itumike kwa mazingira yake.

Mkurugenzi Mkuu wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, Rais Samia amependekeza kuongezwe wigo wa maeneo mapya ya ushirikiano na Vatican ikiwamo uhamilishaji na mafunzo ya ufundi stadi.

Kadhalika, Rais Samia anazungumza na Makamu wa Rais wa kampuni ya Marekani ya Philip Moris kuhusu ununuzi wa tumbaku za Tanzania na ushirikiano wa ujenzi wa kiwanda cha sigara mkoani Morogoro.

Katika ziara ya Norway, Tanzania Rais inasaini hati mbili za makubaliano pamoja na mkataba mmoja na miongoni mwake ni eneo la kuongeza usalama wa chakula na kilimo.

Anasema katika kongamano la biashara linalowakutanisha wafanyabiashara wa Norway na Tanzania, Rais ananadi fursa za uwekezaji kwenye kilimo, mifugo, uvuvi, utalii, mafuta na gesi, usafirishaji na nishati jadidifu.

Mambo mengine ambayo Norway imekubali kushirikiana na Tanzania nishati mbadala, kukabiliana na athari za mabadikiko ya tabianchi, uchumi wa bluu, kuimarisha mifumo ya kukusanya mapato na kuwezesha wanawake kiuchumi.



# Mama alivyokomesha jinamizi la uzazi kuwa sababu ya vifo vya wajawazito

**NA GAUDENSIA MNGUMI**



Rais Samia Suluhu Hassan, akihutubia wabunge Dodoma, Aprili, 2021. **PICHA: NIPASHE**

VIFO vya uzazi ni jambo linalomgusa na kumuumiza karibu kila mwanamke. Linaongeza uchungu hasa mama anapofikiria kuwa ujauzito na uzazi ni sababu ya kifo chake.

Lakini Rais Samia Suluhu Hassan, ameimarisha juhudi zenye mafanikio za kumlinda mjamzito ili kujifungua salama, kumlinda na kumtunza mtoto wake.

Ndiyo maana wakati Rais Samia, analihutubia bunge mwaka 2021, anawaambia wawakilishi wa wananchi kuwa ni mmoja wa watu wanaoumizwa mno na vifo vya wajawazito na wazazi.

Katika hilo anaahidi kumlinda mjamzito na mwanawe aliye tumboni na hata akijifungua ili wote wawe salama na kufurahia maisha.

Miaka mitatu ya Mama wa Taifa, Rais Samia imeshuhudia kupungua vifo vya uzazi kutoka wanawake 556 katika kila vizazi hai 100,000 hadi 104 mwaka 2022.

Vifo vya uzazi ni kifo chochote kinachotokea wakati wa ujauzito au ndani ya miezi miwili baada ya kujifungua.

Kwa Tanzania hali ilikuwa si njema kwani katika vizazi 100,000 hai kinamama 556 walipoteza maisha, ilikuwa ni uchungu na kwa lugha ya mtaani uzazi ulichukuliwa kama kitanzi au mguu kaburini. Zilikuwa taarifa zilizosikitisha wenza, familia na ndugu wa kinamama waliofariki kwenye uzazi.

Oktoba mwaka jana wakati anazindua ripoti ya utafiti wa afya ya uzazi na mtoto na viashiria vya malaria Tanzania ya mwaka 2022, Rais anasifu hatua zilizofikiwa akisema, mwaka 2015/16 idadi ya vifo ilikuwa 556 lakini namba zimeshuka kufikia vifo 104 kwa vizazi 100,000.

Matokeo hayo yameonyesha kuwa Rais Samia amekuwa kinara katika kuhakikisha afya za mjamzito, mzazi na mtoto wake baada ya kujifungua zinalindwa kwa kuwawekea miundombinu wezeshi na kuwapatia wataalamu wakufanya kazi kwa ubora kote nchini.

Kama anavyosema kuwa vifo vinavyotokana na uzazi vinamuuma, mama au mtoto ama wote wawili kufariki, havikubaliki kwa sababu njia za kuvizuia zipo na zinatekelezeka, kwa kuongeza zaidi jitihada na ubunifu wa kuwa na taifa lenye uzazi salama.

Lengo endelevu la Umoja wa Mataifa namba tatu (SDG 3), linataka mataifa kuwalinda, kuwahakikishia maisha, afya bora na kukuza ustawi kwa raia wa umri wote kuanzia watoto, vijana na wazee.

Aidha, linaagiza kuwa ifikapo mwaka 2030, dunia iwe imepunguza idadi ya vifo vya uzazi hadi chini ya 70 kwa kila wanawake 100,000 wanaojifungua vizazi hai.

Kadhalika, serikali zinahimizwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi kwa wote, ikijumuisha kupanga uzazi, taarifa na elimu na kujumuisha afya ya uzazi katika mikakati na programu za kitaifa.

"Tukilinganisha na shabaha ya SDGs inayotuagiza mpaka 2030 vifo vitokavyo na kinamama wakati wa kujifungua visizidi 70 kwa kila 100,000, safari yetu inaweza kufikia lengo hilo," anasema Rais.

Katika kuendelea kumsaidia mjamzito na mtoto, Rais Samia mapema 2022, alizindua Mfumo wa usafirishaji wa dharura kwa wajawazito na watoto wachanga, M-MAMA unaolenga kunusuru maisha ya wajawazito na watoto.

Mfumo wa M-MAMA unaokoa maisha kwa kuimarisha taratibu za rufaa na usafiri wa dharura kwa gharama nafuu kwa kutumia teknolojia ambao unamtoa mjamzito au mtoto mchanga kutoka vituo vya fya vya kata na kumpeleka kwenye hospitali za rufaa za wilaya kwa matibabu na huduma bora zaidi Dokta John Jingu ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, anayezungumzia mafanikio ya kupunguza vifo hivyo.

> "Kama anavyosema kuwa vifo vinavyotokana na uzazi vinamuuma, mama au mtoto ama wote wawili kufariki, havikubaliki kwa sababu njia za kuvizuia zipo na zinatekelezeka, kwa kuongeza zaidi jitihada na ubunifu wa kuwa na taifa lenye uzazi salama.

Anasema mafanikio ya kupunguza vifo vya uzazi ni matokeo ya kujenga miundombinu bora ya afya zikiwamo wodi za kisasa za wazazi, kuweka vifaa na kusomesha madaktari na wataalamu wa afya ili kuwahudumia kwa weledi.

Katika hatua nyingine, mafanikio ya kupunguza vifo vya wazazi kwa asilimia zaidi ya 80, iliyoifanywa na Tanzania imeigusa Nigeria ambayo maofisa wake mwezi uliopita wanaitembelea Tanzania kujifunza mbinu zilizofikiwa.

Viongozi hao kutoka Nigeria wakiongoozwa na Kamishna wa Afya Profesa Baba Gana, wanafika nchini baada ya taifa kuwa kinara wa kupunguza kwa kasi vifo vya wazazi na watoto katika Ukanda wa Kusini ya Jangwa Sahara.

Tanzania inaelekea kufikia lengo endelevu namba tatu la Umoja wa Mataifa la kupunguza vifo hivyo hadi chini ya 70 kabla ya mwaka 2030.

**TIBA KIBOBEZI**

Rais katika kipindi cha miaka mitatu amewekeza kwenye tiba za kibobezi. Kwa njia hiyo Watanzania wengi wameokolewa na matatizo ya moyo katika huduma za kibingwa zinazotolewa nchini.

Kwa mfano mapema mwaka huu Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, anaeleza kuwa wagonjwa wa moyo zaidi ya 800 wamefanyiwa upasuaji mkubwa hapa nchini kazi ambayo ilikuwa ifanyike nje ya nchi.

Akizungumza katika kusanyiko la wataalamu wa magonjwa ya moyo mwanzoni mwa mwaka huu, anaeleza kuwa wagonjwa wengine zaidi ya 2,000 walipasuliwa moyo kwa njia ya tundu dogo.

Ni upasuaji unaofanywa kwenye chumba maalumu chenye kazi mbalimbali kama kupima moyo, kuupasua na kuuwekea vifaa saidizi. Maabara hiyo huitwa 'catheterization laboratory' au cathlab'.

Dk. Mpango anasema ni kazi inayofanyika katika kipindi cha miaka miwili ndani ya Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) iliyoko ndani ya Hospitali ya Taifa Muhimbili

**TIBA UTALII**

Halikadhalika, serikali ya Rais Samia, imeendeleza tiba utalii. Akilizungumzia hilo Makamu wa Rais anasema wagonjwa wa moyo zaidi ya 200,000 wametibiwa na wataalamu wa JKCI kwa kipindi cha miaka miwili ambapo kati yao 2,400 wanatoka nchi za jirani.

"Wanatoka mataifa ya Comoro, Congo DRC, Kenya, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Uganda pamoja na Zambia." Anasema.

Anasema JKCI sasa ni taasisi ya umma inayoongoza katika kutoa huduma za matibabu ya moyo Afrika Mashariki na kati, hivyo kuwavutia wanataaluma kutoka nchi kama Malawi, Zambia na Rwanda kujenga na kuongeza ushirikiano.

Anazungumzia mapato akisema, serikali imeokoa Shilingi bilioni 63 zilizokuwa zitumike kwa ajili ya matibabu ya moyo nje ya nchi, ambazo bila shaka zimetumika kwenye miradi ya maendeleo .

JKCI inakuwa sehemu ya tiba utalii kwa kuwa inaingiza nchini wagonjwa wanaotumia huduma za afya kwa kulipia fedha za kigeni, kadhalika waishi kwenye hoteli, kutembelea maeneo mbalimbali na kununua bidhaa yote hayo yakiendeleaza utalii na kuitangaza Tanzania kimataifa.

# Walioenguliwa warejeshwa shule, mabinti na wanavyuo wakifaidi sapoti ya 'mama'



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan (kulia) na Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa (kushoto), wakivuta pazia kuashiria uzinduzi wa shule za awali, msingi na sekondari zilizojengwa nchini kupitia Mradi wa Uhimarishaji, Ufundishaji na Ujifunzaji (BOOST) na Mradi wa Kuimalisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP), Oktoba mwaka jana, mkoani Singida. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

TAREHE ya leo, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anatimiza miaka mitatu tangu alipokula kiapo kuongoza nchi, siku chache baada ya kifo cha mtangulizi wake, hayati Dk. John Magufuli.

Katika kipindi hicho cha miaka mitatu ya uongozi wake, yapo mengi ambayo kiongozi huyo wa nchi ameshafanya kwenye sekta mbalimbali, lengo likiwa ni kuwaletea Watanzania maendeleo.

Hapo eneo mojawapo ambalo ni katika sekta ya elimu, ambayo, kimsingi ni uti wa mgongo wa taifa. Nikiri, kwa rekodi yake amejitahidi kuendeleza mengi ya watangulizi, ikiangaliwa kuanzia kupanua fursa, hadi kwenye kuboresha elimu katika ngazi zote, shuleni hadi vyuoni.

Eneo stahiki ambalo linafanyiwa kazi ni katika kuboresha sura mbalimbali, ili iweze kuwa na manufaa kwa wanafunzi wa jinsi zote wakiwamo wa msingi hadi vyuo vikuu.

Hadi sasa ana ubunifu wake katika maboresho ya kuwapo shule za sekondari 26 za wasichana za masomo ya sayansi na hisabati zinazojengwa kila mkoa, ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo hayo katika ngazi ya sekondari kitaifa.

Pia, sekondari hizo kwa sasa ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi ili zikikamilika ziweze kuwanufaisha wasichana.

Lengo la kujenga sekondari hizo ni kutaka kuhamasisha wasichana kupenda masomo ya sayansi ambayo wengi wao wamekuwa wakiyakimbia.

Kwa hiyo, ni wazi kwamba ujenzi huo ukikamilika unaweza kunufaisha wasichana wengi na hivyo nchi kuwa na wataalamu wengi wa kike wa fani mbalimbali kwa miaka ijayo.

**'SAMIA SCHOLARSHIP'**

Katika jitihada zake za kuboresha elimu kwa watoto wa kike, ameanzisha ufadhili maalum kwa wahitimu elimu ya kidato cha sita wanaofanya vizuri katika masomo ya sayansi.

Rais anagharamia elimu ya juu kwa asilimia 100 kupitia mpango huo wa 'Samia Skolashipu' ambayo mwaka wa masomo 2023/24 wanafunzi 640 walifaidika.

Ufadhili huo ni kwa masomo ya ngazi ya shahada ya kwanza kwa wanafunzi waliopata ufaulu wa juu katika mitihani ya kidato cha sita mwaka 2023 inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) katika tahasusi za Sayansi na kuchaguliwa kujiunga na Programu za Sayansi Teknolojia, Elimu Tiba na Hesabu katika vyuo vikuu nchini.

Katika mwaka wa masomo 2023/24, Wizara ya Elimu ilitenga zaidi ya Sh. blioni 6 kuwezesha utekelezaji wa mpango huo.

Inaelezwa kuwa, kwa miaka miwili sasa, idadi ya wanafunzi watakaokuwa na mpango huo, itakuwa imefikia wanafunzi 1276.

**MIKOPO KWA DIPLOMA**

Pia, chini ya uongozi wake, Rais ameshusha mikopo hadi kwa wanafunzi wanaodahiliwa kusoma diploma katika fani za kipaumbele kitaifa kwa mwaka wa masomo 2023/24.

Fani hizo za kipaumbele zimegawanya katika maeneo saba, ambazo ni; Afya na Sayansi Shirikishi, kwa upande wa elimu, Diploma ya Ualimu wa masomo ya Fizikia, Hisabati na Amali.

Vilevile kuna fani za Usafiri na Usafirishaji, Uhandisi wa Nishati, Madini na Sayansi ya Ardhi, Kilimo na Mifugo, huku

serikali hiyo ya awamu ya sita, ikiamua kufuta tozo ya asilimia sita mikopo kutoka kwa wanufaika wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB).

**WATORO WARUDI SHULE**

Katika hatua nyingine, Rais ameruhusu wanafunzi waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo mimba kurudi shuleni kuendelea na masomo.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka jana, wanafunzi 18,708 waliopata mimba walikuwa wamerudi shuleni maeneo mbalimbali nchini tangu Rais alipotoa maelezo hayo mwaka 2021.

Uamuzi huo wa Rais ilitokana na kutambua changamoto mbalimbali zinazomkabili mtoto wa kike na kushindwa kutimiza ndoto zake katika elimu.

Inaelezwa kuwa, miongoni mwa changamoto ni wazazi na walezi kutotenga bajeti na kutoa huduma ili kukidhi mahitaji na wanaoingia kwenye vishawishi na kusababisha mimba za utotoni.

Kwamba watoto wa kike wanaingia kwenye ndoa za utotoni kwa sababu sio chaguo la kwanza, hivyo serikali imeona warudi shuleni kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

# WADAU WAMPA '5' USTAHIMILIVU KISIASA USTAWISHAJI, KUSUKA DEMOKRASIA UPYA

**INATOKA UK.11**

"Tunaona uchumi wetu umeanza kuinuka. Tunaenda kwa kasi nzuri," anasema Mchungaji Matonya.

Anaeleza kuwa kisiasa, Rais Samia alichukua nchi kukiwa hakuna uhuru wa kujieleza wala mikutano ya hadhara, ambayo ameifungulia, pia kulikuwa na chuki kubwa miongoni mwa vyama, ufinyu wa kujieleza, kufungwa kwa mikutano ya hadhara, watu walifungwa pia na kushtakiwa.

Yote aliyafungua huu ni ujasiri mkubwa na pia kuonyesha tofauti kiuongozi," anasema Mchungaji Matonya.

"Rais Samia ameonesha ukomavu kwa kuunda kikosi cha kumshauri na kukubali kuupokea na kuufanyia kazi maoni ya timu hiyo. Amefungua jukwaa la mjadala ndani ya vyama," anaongeza.

Anaongeza kuwa ameaunda kikosi kikakusanya maoni na anayafanyiakazi, akisema kwake ni dhahiri anafanya vizuri na kuwataka wanawake wajivunie kwamba wanaweza naye Rais Samia, amefungua huo mlango wa dhana hiyo.

Kuhusu miradi mikubwa ukiwamo ujenzi wa bwawa la umeme la Julius Nyerere na reli ya kisasa SGR, pamoja na ukarabati ya miundombinu ya nishati, Mchungaji Matonya anasema ni ujasiri mkubwa kuendeleza miradi hiyo nchi ikiwa imeyumba kiuchumi.

"Ni jambo la kumshukuru sana Mungu. SGR alipokuwa anaichukua hakukuwa na fedha, angeweza kuiacha lakini ameibeba na tunaona maendeleo makubwa hadi majaribio yanafanyika. Hakuna kilichoachwa nyuma."

Katika nyanja za kimataifa, anasema aliingia madarakani Tanzania ikiwa haina mahusiano mazuri na nchi nyingine, ambayo ameyarejesha na kuyaimarisha.

Anasema kuimarika kwa mahusiano hayo kumevutia wawekezaji na hivyo kuzalisha ajira na kuongeza mzunguko wa fedha kwenye uchumi wa nchi.

**KUONGEZA NGUVU**

Matonya anawataka watendaji kutembea mwendo wa Rais Samia ili yale ambayo Watanzania wanayataka wayaone.

"Kunahitajika marekebisho ya sheria ambazo zilirekebishwa kwa nia ya kuminya uhuru wa kujieleza na vyama vya upinzani. Sheria za uchaguzi na ile ya huduma za vyombo vya habari inabidi zirekebishwe ili watekelezaji wazisimamie."

"Namwona Rais ana nia nzuri, lakini nina wasiwasi na watendaji wake hawaendi na kasi kama yake, wapeleke mapendekezo ya muswada ili kuwepo na marekebisho ya sheria hizi...ukimwacha yeye kama Mwenyekiti wa CCM na Makamu wake, watendaji wengine bado wana mambo yao bado."

Anawataka pia watendaji na 'machawa' wasimtukuze sana Rais kiasi cha kumkosea Mungu akikosoa kauli kama 'Rais ametoa fedha'.

Anakumbusha Rais anafanya juhudi kwa kuwa yeye ni kiongozi anayeshirikiana na wananchi kujenga Tanzania Bara na Visiwani.



# Wachimba kokoto, kifusi katikati ya Jiji, Jafo atoa maagizo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, ametoa siku 14 kwa ofisi ya madini Mkoa wa Dodoma, Jiji na Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), kufanya tathmini ya uharibifu wa mazingira uliosababishwa na shughuli za uchimbaji kokoto na kifusi katikati ya Jiji kinyume na sheria ya mazingira.

Pia ameagiza baada ya tathmini hiyo kukamilika akabidhiwe taarifa ili atoe maamuzi ambayo yatasaidia kulinda mazingira kutokana na uharibifu unaofanywa.

Alitoa maagizo hayo juzi jijini hapa baada ya kufanya ziara ya kukagua shughuli za uchimbaji madini ya ujenzi aina ya kokoto na kifusi katika eneo la Iyumbu na Njedengwa.

Alisema sheria ya mazingira inakataza shughuli za uchimbaji wa madini hayo ndani ya Jiji, hivyo anatoa wiki mbili kwa NEMC, ofisi ya madini mkoa na Jiji kufanya tathmini na kumpatia ripoti ya ushauri ili atoe maamuzi.

Aidha, alisema kitendo cha Ofisi ya Madini Mkoa wa Dodoma kutoa leseni ya uchimbaji huo ni kosa, hivyo wanapaswa kuona namna ambavyo uchimbaji huo utasitishwa ili kulinda mazingira.

"Ni ajabu sana ofisi ya madini na Jiji kushiriki kuharibu mazingira kwa kutoka leseni na vibali vya uchimbaji wa kokoto na kifusi. Lazima mfanye tathmini ili kubaini milima yote iliyopo ndani ya Jiji kama hivi ambavyo watu wanachimba madini haya na kuharibu mazingira ili tuweze kuvilinda." Alisema Jafo.

Ofisa Maliasili na Mazingira wa Jiji la Dodoma, Dk. Vedastus Milinga, alisema maeneo hayo awali yallikuwa na leseni ya uchimbaji.

Alisema lakini hivi sasa wamesitisha lakini watu kuendelea kuchimba kokoto na kifusi, hivyo watakwenda kufanya tathmini hiyo ili kubaini maeneo yote ambayo bado uchimbaji unafanyika.

Awali, Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Dodoma, George Kaseza, alisema awali maeneo hayo kabla ya Dodoma kuwa Jiji yalikuwa na leseni ambazo zilitolewa na ofisi yao kwa watu ambao wanaendesha shughuli za uchimbaji kokoto na kifusi kwa ajili ya ujenzi.

# Upatikanaji wa maji mjini wafikia 90%, vijijini 79%

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UPATIKANAJI wa maji kwa wananchi maeneo ya mijini umefikia asilimia 90.1, vijijini ni asilimia 79.6, huku serikali ikiendelea kuweka mikakati ya kumtua mwanamke ndoo kichwani.

Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Wanyenda Kutta, alieleza hayo jana wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Maji Duniani kwa niaba ya Waziri wa Maji, Jumaa Aweso.

Alisema hatua hiyo imefanikiwa kupunguza umbali wa upatikanaji wa maji, wananchi wengi wanapata maji karibu na wanapoishi.

Alisema pia imesaidia kupunguza muda uliokuwa ukipotea kwa ajili ya kutafuta maji na wananchi wanafanya shughuli nyingine.

Vilevile alifafanua kuwa upatikanaji wa uhakika wa maji ni nyenzo muhimu kwa maendeleo hasa kwa wanawake ambao wamekuwa ni watekelezaji wa shughuli muhimu majumbani.

Kutta alisema Wiki ya Maji Dunuani imeanza Machi 16 hadi Machi 22 na kutakuwa na shughuli mbalimbali ikiwamo matembezi, uwekaji wa mawe ya msingi na uzinduzi wa miradi ya maji nchini.

Pia alisema Machi 18, mwaka huu itakuwa ni Siku ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) itatoa tathmini ya utendaji wa mamlaka za maji, pia itakuwa ni mkutano wa mapitio ya sekta ya maji nchini.

"Matukio hayo yatafanyika na itakuwa ni kazi endelevu katika kuhakikisha serikali inamtua mama ndoo kichwani, maji ni uhai tulinde vyanzo vya maji na kuviendeleze, pia kulinda miundombinu ya maji hapa nchini kwa faida ya vizazi vyetu," alisema.

Aliitaka jamii kutambua umuhimu na thamani ya maji katika maisha ya binadamu na uchumi wa dunia kwa ujumla.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Taifa wa Maji, Haji Nandule, alisema kuwa Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akifanya kazi kubwa ya kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri (kulia), akiwakabidhi cheti Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (MUWSA), Mhandisi Kija Limbe (kushoto) na Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Prof. Jafar Kideghesho (wa pili kushoto), baada ya kutangazwa washindi wa pili kwa mamlaka inayotoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Utafiti: Vifaa kutoka ughaibuni 'vinakula' umeme

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

UTAFITI uliofanywa na wataalamu wa matumizi bora ya nishati ya umeme nchini umeonesha kuwa vifaa vingi vinavyoingizwa nchini vinatumia kiasi kikubwa cha nishati ya umeme, hali ambayo inachangia kuongeza gharama kwa watumiaji.

Mtaalamu mshauri wa mradi wa matumizi bora ya umeme kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Robert Washija, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma kwenye hafla ya uzinduzi wa wazo la ubunifu wa nishati safi ya umeme nchini.

Washija alisema katika utafiti waliofanya mwaka jana unaonyesha kuwa vifaa vingi vya umeme vinavyoingizwa nchini vinatumia nishati nyingi ya umeme na kuwaongezea gharama wananchi.

Alisema vifaa hivyo vimeonekana kuwa na kiwango kikubwa cha matumizi ya nishati ya umeme jambo ambalo linawaongezea gharama watumiaji wa nishati hiyo.

Alisema lengo la kuanzisha shindano hilo la ubunifu ni kupata mawazo yatakayosaidia kupunguza matumizi makubwa ya nishati ya umeme nchini, ili kulinda pato la wananchi.

Kadhalika alisema kuna baadhi ya watu wananunua vifaa vya matumizi ya nishati ya umeme vyenye gharama ndogo, lakini matumizi yake ya umeme yanaweza kuwa mara tano ya yule aliyenunua kifaa kama hicho kipya kwa bei ghali.

Alivitaja vifaa hivyo vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi ambavyo baadhi vinatumia umeme mwingi kuwa ni majokofu, viyoyozi, kompyuta.

Pia alisema kutokana na Tanzania kuingia katika uchumi wa kati inatakiwa kuwa na ubunifu wa kuendelea kutumia teknolojia za kisasa ili kuongeza uchumi.

Alisema elimu inahitajika kuwafikia watumiaji wa nishati hiyo kutokana na kuendelea kuwapo kwa vifaa hivyo vyenye matumizi makubwa ya umeme.

Ofisa Mawasiliano wa UNPD, Jolson Masaki, alisema shindano hilo la wazo bunifu lililozinduliwa jana litakuwa la mwezi mmoja na litashirikisha Watanzania wote bila kujali rika la mhusika.

Masaki, alisema shindano hilo limefadhiliwa na Serikali ya Ireland, Shirika la UNDP na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU) kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kusimamia ubunifu wa nishati bora ya umeme.

Alibainisha kuwa katika ufadhili huo, Ireland wamechangia Euro 600,000, UNDP wamechangia Euro milioni moja na EU wamechangia Euro milioni nane na kufanya jumla ya fedha hizo kuwa ni Euro milioni 9.6.

Aliongeza kuwa wa mchujo wa kwanza wa shindano hilo unatarajiwa kuwapata watu 20 ambao watakaa kambini kwa muda wa wiki moja, ambapo bunifu hizo zitapitiwa na kuwapata washindi 10 na waliobaki watapewa Sh. milioni tano kila moja .

Alisema kwa washindi 10 bora watapewa Sh. milioni 10 kila moja na mawazo hayo bunifu yatahifadhiwa ili kuisaidia jamii katika kutatua tatizo la nishati bora.

Alieleza kuwa shindano hilo litashirikisha pia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) pamoja na Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Nishati.

Mwakilishi wa Wizara ya Nishati, Collins Lwanga, aliwashukuru shirika hilo kwa kusaidia bunifu hizo akisema zitasaidia kuboresha maisha ya wananchi.

Lwanga alisema serikali imekuwa ikiendelea na kutoa elimu ya matumizi ya nishati bora na imeshirikiana na kampuni za kutumia gesi katika kusambaza majiko hayo kwa lengo la kupunguza uharibifu wa mazingira.





# Migogoro ya ardhi yahatarisha maisha ya wakazi wa Chunya

**Na Nebart Msokwa,**
CHUNYA

WANANCHI wilayani Chunya mkoani Mbeya, wamesema wanakabiliwa na migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikihatarisha hali ya amani, kutokana na wengi wao kukosa elimu ya matumizi sahihi ya ardhi.

Wamesema kutokana na hali hiyo kumekuwa na mwingiliano wa matumizi ya ardhi hali ambayo inakuwa chanzo cha migogoro ambayo inakwamisha shughuli zao za uzalishaji.

Mwakilishi wa wakulima wilayani humo, Faraja Kyando, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha wadau wa upangaji wa matumizi ya ardhi kilichokuwa kimeandaliwa na Taasisi ya MIICO inayotekeleza mradi wa uendelezaji wa upatikanaji wa ardhi bora kwa wazalishaji wadogo katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema katika wilaya hiyo kuna migogoro kati ya wakulima na wafugaji, wakulima na wachimbaji wa madini hasa dhahabu na wakulima na hifadhi za taifa.

Alisema migogoro hiyo wakati mwingine imekuwa ikisababisha uzalishaji wa mazao kupungua kutokana na wakulima kuogopa kuwekeza fedha zao kwenye shughuli hiyo.

“Tunaiomba serikali na wadau wote mliopo hapa, mwendelee kutuelimisha kuhusu matumizi bora ya ardhi kwa sababu kumekuwa na mwingiliano mkubwa wa shughuli zetu, yapo maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji lakini hawapeleki mifugo huko badala yake wanaleta kwenye mashamba,” alisema Faraja.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, aliwataka wataalamu wa halmashauri hiyo kushirikiana na wadau mbalimbali kuwaelimisha wananchi kuhusu matumizi sahihi ya ardhi na madhara ya migogoro.

Alisema wilaya hiyo imekuwa ikikabiliwa na migogoro ya mara kwa mara baina ya wananchi kulingana na shughuli zinazotekelezwa kwenye maeneo hayo.

“Tumieni ujuzi na elimu yenu, tumieni mikusanyiko na majukwaa mbalimbali kutoa elimu kwa wananchi wetu, waelimisheni watendaji na wenyeviti wa vijiji, wawe na elimu sahihi kuhusu ardhi ili kuepuka kuwa chanzo cha migogoro katika meneo yao,” alisema Mwanginde.

Kaimu Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Athuman Bamba, aliwataka watendaji wa vijiji kutoa ushirikiano kwa taasisi zinazotoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya ardhi.

Alisema serikali peke yake haiwezi kutatua migogoro yote inayoibuka na badala yake inashirikisha wadau wa sekta binafsi ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Ofisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya hiyo, Cuthbert Mwinuka, alisema wameandaa mkakati mbalimbali ya kupambana na migogoro ya ardhi ikiwa ni pamoja na kuanzisha mashamba ya mifugo ili kuwafanya wafugaji wasitembeze mifugo yao.

Vilevile alisema wameandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ambayo ndiyo yatakayotumika kuainisha maeneo ya makazi, kilimo na mifugo ili kuepusha mwingiliano wa shughuli hizo.

Ofisa Mradi wa Taasisi ya MIICO, Glory Mdindile alisema wanalenga kushirikiana na Serikali pamoja na wadau wengine kwenye masuala ya ardhi ikiwa ni pamoja na kufahamu shughuli mbalimbali zinazofanywa na wadau.




Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, akishikiliwa mkono na wananchi ambao walijumuika pamoja katika kuwaokoa baadhi ya watu ambao walikwama katika makazi yao kufuatia mafuriko makubwa yaliyosababishwa na Mto Miombo kujaa na kuharibu miundombinu ya madaraja, barabara na makazi ya watu, zaidi ya kaya 156 zimekosa makazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC aagiza uongozi ushirika Njombe kuanzisha viwanda

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, ameutaka uongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Njombe (NJORECU) kuandaa mpango wa kuanzisha viwanda ili kwenda na kasi ya mabadiliko ya teknolojia badala ya kuishia kuuza mazao pekee yatokanayo na nafaka.

Kasongwa aliyasema hayo wakati akizungumza na wanachama wa chama hicho kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa chama hicho uliofanyika mjini hapa.

Hata hivyo alisema vyama hivyo havipaswi kujifungia wilayani humo badala yake watoke kwenda kujifunza.

“Kwa maana tutoke kwenye uzalishaji wa kawaida twende kwenye viwanda, ningependa sana kwenye mkutano unaokuja tuwe na wadau wakubwa wakubwa wa viwanda ili kusaidia kuleta tija,” alisema Kasongwa.

Alisema kuwa ni vema pia kukatatuliwa changamoto zinazowakabili wanachama wa vyama vya ushirika ambao wametapeliwa fedha zao.

“Bado tunachangamoto kuna vyama vya ushirika vimewatapeli watu hela zao na bado hawajarudishiwa, vyama vipo kama vinataka kufa lakini bado vinamadeni ya watu wengi ambao ni wazee,” alisema Kasongwa.

Mwakilishi wa Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini, Juma Mokili alikitaka chama hicho kujiendesha kibiashara.

Mwenyekiti wa AMCOS ya Ilembula, Justine Mwinuka, alisema Njombe inacheleweshwa kutokana na madeni ambayo yanadaiwa katika vyama vya ushirika.

Mwenyekiti wa NJORECU, Stephano Luoga alisema wameazimia kwamba watu ambao wanadaiwa fedha za wanachama wafuatiliwe ili wazirudishe lakini waliokufa madeni yatafutwa.

# ‘Wazazi, walezi changieni chakula shuleni kuongeza ufaulu’

**Na Nebart Msokwa,**
TUKUYU

WAZAZI na walezi wilayani Rungwe mkoani Mbeya wametakiwa kuendelea kuchangia chakula cha mchana kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, ili kuongeza kiwango cha ufaulu na kukabiliana na tatizo la udumavu.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Rungwe, Ally Kiumwa, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha tathmini ya mkataba wa lishe kilicholenga kujadili mwenendo wa lishe katika wilaya hiyo.

Kiumwa alisema lengo la serikali ni kuhakikisha watoto wanapata lishe bora ili kuwajenga kiafya hatua itakayosaidia kuwa na nguvu kazi ya kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli na miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema lishe bora kwa watoto pia itasaidia kuwa na viongozi bora kwa baadaye watakaosimamia vyema shughuli mbalimbali za uzalishaji mali pamoja na kuiongoza nchi.

“Kimsingi ni ngumu sana kwa mwanafunzi kukaa shuleni kuanzia asubuhi mpaka jioni na hajala kitu, ukitaka kuthibitisha hili siku moja andaa kikao cha wazazi kuanzia asubuhi mpaka jioni bila kuwapa kitu cha kula halafu waulize wanajisikiaje, baada ya hapo ndio utajua kwanini serikali inasisitiza umuhimu wa wanafunzi kupata chakula shuleni,” alisema Kiumwa.

Aliwataka viongozi pamoja na watendaji wote ngazi ya kata kuchukua suala la lishe kama ajenda ya kudumu kwa kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi kwenye kila mikutano wanayofanya kwenye maeneo yao.

Ofisa Lishe wa wilaya hiyo, Halima Kameta alisema hadi sasa ni asilimia 83.7 pekee ya wanafunzi wilayani humo wanapata chakula shuleni.

Alisema uwepo wa uhakika wa chakula kwa wanafunzi shuleni utasaidia pia kupunguza kiwango cha utoro kwa wanafunzi kwa maelezo kuwa wengi huwa wanarudi nyumbani wanapojisikia njaa ili wakale huko.

Mmoja wa wazazi waliohudhuria kikao hicho Lugano Jackson, alipendekeza halmashauri hiyo kutunga sheria ndogo itakayosaidia wazazi kushiriki katika uchangiaji wa chakula shuleni na kuwachukulia hatua wote watakaokaidi.



# Wanaoishi maeneo hatarishi, bondeni waagizwa kuhama

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, amewataka wakuu wa wilaya na kamati za maafa kutoa tahadhari za kuhama kwa wananchi wanaoishi maeneo hatarishi, ili kuepukana na maafa wakati wa mvua za masika.

Aliyasema hayo jana ofisini kwake wakati wa ufunguzi wa mkutano wa wenyeviti wa kamati za maafa za wilaya na kamati za wataalamu wakati wa kujadili mwelekeo wa mvua za masika zilioanza kunyesha.

Aliwataka kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wanaoishi mabondeni na katika njia za maji ili wahame mapema kabla ya athari kutokezea.

Aidha, aliwashauri wenyekiti hao kushirikiana na masheha katika suala zima la usafi wa mitaro, hasa ile inayopitisha maji ya mvua ili kujiweka tayari kwa mvua hizo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja, Hamida Mussa Khamis, aliwataka wananchi kupokea maelekezo ya kuhama mapema katika maeneo ya mabondeni, ambayo huwaletea athari ya kupoteza maisha na mali zao na kutafuta maeneo mengine.

"Naendelea kuwaomba wananchi kukubali kuhama katika maeneo hatarishi na kufuata maelekezo kwa sababu wao ndiyo wanaopata athari," alisema Hamida.

Mkurugenzi Mtendaji Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa, Makame Khatibu Makame, alisema lengo la kikao hicho ni kupata taarifa za mwelekeo wa mvua za masika, kujiandaa kwa kupunguza athari katika maeneo hatarishi.

Alisema suala la maafa ni suala mtambuka, hivyo kila mmoja anapaswa kusimama katika nafasi yake ili kutekeleza majukumu.

Mtaalamu kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) Kanda ya Zanzibar, Hassan Khatib Ame, akiwasilisha mada ya mwelekeo wa mvua za masika ya mwaka 2024 katika visiwa vya Unguja na Pemba, alisema kutakuwa na mvua ya wastani hadi juu ya wastani na athari zinaweza kujitokeza na kusababisha madhara.

# Meya Jiji la Z'bar 'awamwagia maua' Rais Samia, Dk. Mwinyi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MEYA wa Jiji la Zanzibar, Mahmoud Mohammed Mussa, amesema hali ya utoaji wa huduma za ustawi wa jamii hivi sasa Zanzibar imepiga hatua nzuri kutokana na juhudi zilizofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan na Rais Ali Hassan Mwinyi.

Mahmoud aliyasema hayo jana Unguja wakati akifunga mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa ustawi wa jamii wa sekta ya afya na hospitali ikiwa ni shamrashamra za kuadhimisha Siku ya Ustawi wa Jamii Duniani.

Alisema kutokana na juhudi hizo, jamii inapaswa kuwapongeza viongozi hao pamoja na kuwaunga mkono kutokana na jitihada hizo katika kustawisha vizuri maisha ya Wazanzibari na Tanzania kwa ujumla.

Alisema mafunzo hayo yamefanyika vizuri na washiriki watayatumia vizuri kwa faida yao na Wazanzibari kwa ujumla, huku akiwapongeza kwa mwitikio mzuri katika kupata elimu hiyo.

Akiwasilisha mada ya masuala ya ustawi wa jamii, Meneja wa Wataalamu wa Ustawi Jamii katika sekta ya afya, hospitali ya kwenye vituo vya afya katika Jiji la Manchester United, Nanyorry Mwasha alisema maofisa ustawi wa jamii wa Zanzibar wanafanya kazi katika mazingira magumu na wengine pia hawakubariki katika jamii wala katika taasisi.

Hivyo aliwataka kutovunjika moyo, huku akiendelea kuwasaidia katika kutoa elimu ili jamii na viongozi wajue umuhimu wao.

Alisema kuna umuhimu wa kutoa mafunzo hayo kutokana na Rais Mwinyi kufungua milango katika masuala ya kiuchumi na ndiyo maana wakatoa elimu hiyo ili maofisa ustawi kufanya kazi katika jamii iliyowazunguka na kuendeleza ukuaji wa uchumi wa nchi.

Hata hivyo aliwataka kuendelea kujifunza kupitia elimu ya masafa au mafunzo ya muda mfupi na mitandao mbalimbali kwa kujiongezea elimu ili kuwa maofisa bora wa ustawi wa jamii nchini na duniani.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema kuna tatizo kubwa katika baadhi ya taasisi ambapo waajiri wakiwapangia kazi kinyume na taaluma yao waliyosomea, huku wakipewa vitisho kwa kufukuzwa kazi endapo hawatofanya kazi hizo, hali ambayo inadumaza taaluma yao.

Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Wizara ya Afya, Zainab Abdalla Kitole, alisema katika sehemu zao za kazi hawapewi kipaumbele kufanya kazi zao kama inavyotakiwa ikiwamo kutafuta changamoto na siyo kukaaa ofisini kwa sababu kwenye jamii watu wana matatizo mengi na wanahitaji kusaidiwa.



Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Shaaban Ali Othman, akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusiana na uzinduzi wa duru ya kwanza ya utoaji wa vitalu vya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia unaotarajiwa kufanyika Machi 20, mwaka huu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri atoa maagizo mkandarasi Bonde la Chenju 'B'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amemtaka mkandarasi anayejenga miundombinu ya umwagiliaji katika Bonde la Cheju 'B' Wilaya ya Kati Unguja kukamilisha ujenzi huo kwa wakati ili wakulima warudi katika mabonde yao.

Shamata alitoa maagizo hayo jana alipofanya ziara katika bonde hilo kuangalia hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huo unaotekelezwa kwa lengo la kuongeza tija kwenye kilimo cha mpunga.

"Lengo la ziara hii ni kutaka kuona maendeleo ya utekelezaji wa mradi na hatua zilizofikiwa katika ujenzi wa miundombinu hii ili bonde hili lirudi kwenye uzalishaji na wananchi wanufaike na uwekezaji unaofanywa na serikali," alisema Shamata.

Alisema kuwa mradi huo unaohusisha kazi mbalimbali zikiwamo ya uchimbaji wa visima vya maji ikiwamo awamu ya pili katika utekelezaji wa programu ya miundombinu.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutawawezesha wakulima kulima mara mbili kwa mwaka na kuongeza uzalishaji pamoja na kipato chao.

"Nasisitiza hii kazi iishe haraka ili wakulima wetu wasisitishe shughuli zao na kusubiri kwa muda mrefu kwa vile ujenzi huu pia utaisaidia serikali kufikia azma yake ya kuimarisha usalama na uhakika wa chakula nchini," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Ali khamis Juma, alisema pamoja na uimarishaji wa miundombinu kuna haja ya kuwekwa mkakati maalum katika utunzaji wake na kuwataka wafugaji kuacha tabia ya kuingiza mifugo yao katika mabonde yenye miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili ya malisho.

Juma alisema kwa kufanya hivyo kunachangia uharibifu wa miundombinu hiyo sambamba na kuleta migogoro baina ya wakulima na wafugaji mambo yanayochangia kurudisha nyuma uzalishaji.

Mradi unaotekelezwa na mkandarasi kampuni ya Kolon kutoka Korea, unategemea kumalizika Novemba mwaka huu, unatekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Exim Korea kwa Dola za Marekani 18.1.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**HAWA HAMISI MTIRA** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE038473** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu mnamo tarehe 19/07/2018. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/382714/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARYAM MBARAK ELJAEDY,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **NISSAN X-TRAIL** Yenye namba za Usajili **T 911 DZD,** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/7542/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FLAVIAN MARCEL JUSTINE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 919 BBA** aina ya Toyota Corona yenye chassis namba **AT2100028797.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KAG/KAR/2400/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SIXBERT ANDREW WILBROAD,** Anatangaza kupotea kwa Kadi ya Pikipiki yenye no za Usajili **MC 859CLT,** CHASSIS NO **MD2B15BY9KWH96167,** ENGINE NO **JVZWKH48155.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/KON/4520/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPH THOMAS LYIMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 571 ALA** aina ya **SCANIA – MODEL 82** yenye Chassis namba **1807457.** Engine namba **5032588.** Yenye umiliki wa Kampuni ya **TOMMY SPADES MANUFACTURING COMPANY LIMITED.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/UBU/39268/2024.**

## KADI ZA PIKIPIKI ZIMEPOTEA

**Africa Academy for Public Health**

Inatangaza kupotelewa kwa kadi za pikipiki zenye namba za usajili:

T692BWB Chasis: MD2PFPFZZUWE70573

T685BWB Chasis: MD2PFPFZZUWE70526

T696BWB Chasis: MD2PFPFZZUWE70574

T934BVV Chasis: MD2DDJKZZUWE81688

T920BVV Chasis: MD2DDJKZZUWE81730

**Kwa yeyote atakayeziona atoe taarifa Kituo cha Polisi. Taarifa: PHQ/DAR/KIN/36184/2024**

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **GOOD NEIGHBORS TANZANIA-MWANZA** iliyopo jengo la olympic,mtaa wa makongoro Mwanza , Sepco Debt Collection & Auctioneering Co,Ltd tutauza kwa mnada wa hadhara Gari aina ya **TOYOTA LAND CRUISER** ,Usajiri namba **T 201 BLF** ,mnada utafanyika Tarehe **21/03/2024,** katika yard yetu iliyopo **NYAMAGANA/BUHONGWA** kuanzia saa Tatu asubuhi,

**MASHARTI YA MNADA**

Mteja atakayebahatika kununua gari hilo gharama zote za kuhamisha umiliki utakuwa ni za kwake na hatochukua gari hilo mpaka atakapo maliza zoezi la kuhamisha umiliki

Mteja atalipa 30% siku ya mnada, 70% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 30% hairudishwi,Gari linauzwa kama lilivyo,Ukaguzi utaanza Tarehe 20/03/2024

**Mawasiliano piga: - 0715-683777/0750548337 info@sepcoauctioneering.co.tz**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**YUDA PETER MUSHI**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 133 CNF(BOXER)** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi **DAR/URA/RB/127732/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RICHARD TIMOTHEO RUTAYUGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI **T 233 CVH.** YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI JALADA NAMBA **PHQ/IRI/IRI/3108/2024.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WILAYA YA KILOMBERO**

**MAHAKAMA YA MWANZO MLIMBA**


**SHAURI LA NDOA/TALAKA NAMBA 17/2024**

**MDAI.........................REUBEN S. MFANGA**

**DHIDI YA**

**MDAIWA...................MARY S. IDAFA**

Mdai REUBEN S. MFANGA na mdaiwa MARY S. IDAFA wanatarajiwa kuwa na shauri la ndoa/talaka tarehe 26/3/2024 kwenye Mahakama ya Mwanzo Mlimba Kilombero, Mdaiwa MARY S. IDAFA anashauriwa kufika Mahakamani bila kukosa, kukosa kwake kutailazimu Mahakama kusikiliza shauri hili kwa upande mmoja.




HEAD OFFICE
Makumbusho Business Complex
P.O.BOX. 21566,
Dar es Salaam-Tanzania

**SoftFinance.**

Mobile. +255(0)717 718 519
+255(0) 22 270 1320
Email : mkopo@softfinance.co.tz
Web : www.softfinance.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

**SOFT FINANCE LTD** INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ILIYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| S\NO. | MKOPAJI/MDHAMINI | DHAMANA | UMILIKI NA ENEO LA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ANNA THIMOTH NYOKA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – MABWEPANDE | J & J RECOVERIES | 02-04-2024 |
| 2 | ZENATHA JUMA MAJALI | PAGALE | MKATABA WA MAUZIANO – TEGETA MASAITI | J & J RECOVERIES | 02-04-2024 |
| 3 | BAKARI HUSSEIN MPINA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – YOMBO KIWALANI | KAZI WORK INTERPRISES | 02-04-2024 |
| 4 | WASHEKE JOSEPH KANYI | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – UBUNGO MAKOKA | KAZI WORK INTERPRISES | 02-04-2024 |
| 5 | JACQULINE LAMECK KIBOGA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – TUANGOMA | KAZI WORK INTERPRISES | 02-04-2024 |
| 6 | ROSE KIBASA | KIWANJA | MKATABA WA MAUZIANO – UBUNGO MAKOKA | KAZI WORK INTERPRISES | 02-04-2024 |
| 7 | VUMILIA RABIEL LEMA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – SARANGA | KAZI WORK INTERPRISES | 02-04-2024 |
| 8 | ASHA JUMANNE LUNAMBA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – KINYEREZI | LEGENDS AUCTION MART | 02-04-2024 |
| 9 | FATUMA RASHID MFAUME | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – BUZA | LEGENDS AUCTION MART | 02-04-2024 |
| 10 | VERONIKA PASTORY KAZI | VIWANJA | HATI – KEREGE BAGAMOYO | LEGENDS AUCTION MART | 02-04-2024 |
| 11 | ALLY MVUNYO KONDO | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – ZINGIZIWA | LEGENDS AUCTION MART | 30-04-2024 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Wanafunzi waonywa tabia kufuata mkumbo kitaaluma

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imetoa mafunzo maalum kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Geita kwa lengo la kuwawezesha kutambua masomo sahihi wanayomudu na fani zinazoendana na masomo hayo katika soko la ajira.

Mafunzo hayo yalitolewa wiki iliyopita mkoani Geita na baadhi ya wafanyakazi wa GGML wakiwamo wanawake wanaounda kundi la GGM Ladies ikiwa ni mwendelezo wa maadhimisho ya sherehe za Siku ya Wanawake Duniani.

GGML Ladies wametoa mafunzo hayo kupitia programu maalum ya ushauri na usimamizi iliyopewa jina la (GGM Mentorship Program) kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi hao wa kidato cha kwanza hadi cha tano kutambua uwezo wao kielimu na malengo waliyojiwekea katika kutimiza ndoto zao.

Akizungumza na wanafunzi hao, Ofisa wa Masuala ya Usafirishaji kutoka Idara ya Rasilimali Watu, Laila Mohamed alisema huo si muda wa wanafunzi kufuata mkumbo katika kuchagua masomo ya kusoma na kufikia malengo yao kimaisha.

"Ili kufikia malengo ya kitaaluma, hiki si kipindi cha kufuata mkumbo... kwamba ukisikia Juma amechukua Baiolojia na wewe unachukua mchepuo wa sayansi. Hiki ni kipindi cha kujitathmini na kujitafakari kwamba ni kitu gani unakimudu ili uchukue masomo sahihi kufikia lengo lako," alisema.

Aliongeza kuwa wanafunzi wengi wamekuwa na changamoto ya kutokuwa na msimamizi au mshauri anayeweza kuwashauri namna ya kujinasua katika changamoto mbalimbali kitaaluma, jambo ambalo GGML imeona ni vyema kujaza nafasi hiyo.

Joscar Rumanyika ambaye ni mhasibu kutoka GGML, alionya wanafunzi hao dhidi ya vitendo viovu vya uvunjifu wa maadili, akivitaja ni kikwazo kwao kutimiza malengo yao kitaalumu.

Joscar aliwataka wanafunzi hao kuwa na uthubutu na kujiamini kwamba hakuna kinachoshindikana ili kufaulu vyema katika masomo yao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wanafunzi hao kutoka shule hiyo, wakiwamo Leonard Martin na Daniel Stanslaus, walisema mafunzo waliyopatiwa na GGML yamewasaidia kutambua namna ya kufikia malengo yao.

Martin (14), ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha pili na mkazi wa Bwanga, mkoani Geita, alisema elimu hiyo inawawezesha kujiandalia maisha mazuri ya baadaye.

Makamu Rais Mwandamizi wa AngloGold Ashanti-GGML - Kitengo cha Ubisa/ Ushirika Afrika, Terry Stron alisema programu hiyo ya mentorship inalandana na malengo ya kampuni hiyo ya kuwekeza kwa vizazi vijavyo kwa kuwa kuwekeza kwa wanafunzi hao ni sawa na kuwekeza kwa jamii ya Geita ijayo.

# Kesi ya Gekul yaanza tena mahakamani

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

KESI ya unyanyasaji inayomkabili Mbunge wa Babati Mjini (CCM), Pauline Gekul, iliyofunguliwa katika Mahakama Kuu Kanda ya Manyara na mfanyakazi wake Hashim Ally, imepigwa kalenda hadi Machi 21, mwaka huu.

Jana, Jaji Devotha Kamzola anayesikiliza shauri hilo, alisema Mahakama hiyo imejiridhisha kwamba hakuna kumbukumbu inayoonesha mrufaniwa (Gekul) amepata hati ya wito wa mahakama hiyo.

Alifikia uamuzi huo wa kuipiga kalenda baada ya wajibu rufani kuieleza mahakama hiyo hawajapokea wito huo.

Alisema kutokana na kutoonekana nyaraka hizo, ni vizuri shauri hilo kuahirisha ili wajibu rufani wapate nafasi ya kuzipitia nyaraka.

Nje ya Mahakama, Wakili Peter Madeleka anayemwakilisha Hashimu Ally, alidai kuwa shauri hilo lilikuwa lianze kusikilizwa jana, lakini isivyo bahati, limeshindwa kuendelea kwa sababu mahakama imeshindwa kutimiza wajibu wake wa kumpelekea wito na nyaraka za rufani mshtakiwa.

Hashim anawakilishwa katika kesi hiyo na mawakili watatu, ambao ni Peter Madeleka, Thadei Lister na John Masanja wakati Gekul anatetewa na Wakili Efrahim Kisanga, akisaidiana na Wakili Melkizedek Hekima.

Katika shauri la msingi, mbunge huyo alifutiwa kesi ya unyanyasaji dhidi ya mfanyakazi wake Hashim Ally na Mahakama ya Wilaya ya Babati baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DDP) kuwasilisha taarifa ya kutokuwa na nia ya kuendelea na shauri hilo.

DPP aliwasilisha taarifa hiyo ya kutokuwa na nia ya kuendelea na kesi hiyo chini ya kifungu cha 91(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai CPA, kinachompa mamlaka ya kufuta kesi yoyote ya jinai katika hatua yoyote kabla ya hukumu ya mahakama na bila kulazimika kutoa sababu za uamuzi huo.

Kesi ya msingi ilifunguliwa na Hashim kupitia kwa Wakili Madeleka, chini ya kifungu cha 128(2) na (4) cha Sheria ya CPA kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2022.

Wakati kesi hiyo inafunguliwa Mahakama ya Wilaya ya Babati, Wakili Madeleka, alidai kifungu hicho kinaruhusu mtu binafsi kufungua kesi ya jinai bila kupitia kwa DPP.

Katika shauri la msingi, Gekul alikuwa anakabiliwa na shtaka moja la shambulio na kusababisha madhara kwa mwili, chini ya kifungu cha 241 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, marekebisho ya mwaka 2022.

Alikuwa anadaiwa kuwa yeye na watu wengine ambao hawako katika malalamiko hayo, Novemba 11, mwaka 2023, mjini Babati, mkoani Manyara, walimwita Hashim na kumweka kizuizini.

Ilidaiwa kuwa huku wakimtishia kwa silaha ya moto, walimvua nguo na kumshambulia kwa kumlazimisha kukalia chupa ya soda ili iingie katika njia yake ya haja kubwa.




Andrew Mazula, Ofisa Utumishi kutoka Idara ya Rasilimali Watu - GGML, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Geita kuhusu masuala muhimu wanayotakiwa kuzingatia ili kufikia mafanikio na malengo yao kitaaluma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wauawa kwa tuhuma kuiba na kuchinja ng'ombe kijijini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATU wanne wanaosadikiwa kuwa ni wezi wa mifugo wameuawa na wananchi, wakituhumiwa kuiba na kuchinja ng'ombe katika Kijiji cha Chikole, wilayani Chamwino, mkoani Dodoma.

Akizungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martin Otieno, alisema watu hao wanadaiwa kuiba ng'ombe wanne ambao waliwachinja bila kuwachuna ngozi na kuwapakia kwenye gari aina ya Toyota Hiace lenye namba za usajili T151 DDJ.

"Wananchi walitilia shaka hilo gari na kuanza kulifuatilia ambapo wahusika walikimbilia porini na wananchi walikuta ndani ya gari mna hao ng'ombe na wakalichoma moto, huku wengine wakiwakimbiza watuhumiwa na baada ya kuwakamata wakajichukulia sheria mkononi na kuwaua watu hao," alisema.

Kamanda huyo alisema hadi sasa watu hao wawili wametambuliwa na wengine bado hawajatambuliwa na miili yao iko katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

"Waliotambuliwa ni Mkazi wa Chang'ombe, Ramadhan Hamis aliyekuwa anafanya kazi machinjio ya mnadani na Mkazi wa Kikuyu, Onesmo Abel ambaye ni muuzaji nyama," alisema.

Kamanda Otieno alisema jeshi hilo linaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuimarisha ulinzi wa mifugo yao kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo.

"Wananchi tushirikiane kufanya doria za masafa mafupi na marefu kupitia polisi jamii ili kubaini na kukamata watu wanaojihusisha na uhalifu na kuwachukulia hatua za kisheria ili kukomesha wizi wa mifugo mkoani Dodoma," alisema.

# NBC YAAHIDI MAKUBWA ZAIDI IKIMKABIDHI GAMONDI ZAWADI

**Na Mwandishi Wetu**

MDHAMINI Mkuu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), imekabidhi zawadi ya pesa na tuzo kwa kocha bora wa ligi hiyo wa mwezi Februari, Miguel Gamond wa Klabu ya Yanga, huku ikiahidi makubwa zaidi katika sekta hiyo ya michezo.

Makabidhiano ya zawadi hizo yalifanyika juzi muda mfupi kabla ya kuanza kwa mchezo kati ya Azam FC dhidi ya Yanga uliofanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kocha huyo kushuhudia timu yake ikikubali kichapo cha mabao 2 -1.

Katika tukio la makabidhiano ya zawadi hizo, ilishuhudiwa Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa Benki ya NBC, David Raymond, akikabidhi tuzo pamoja na mfano wa hundi ya pesa yenye thamani ya Sh. milioni moja kwa Gamondi ikiwa ni mwendelezo wa utaratibu wa mdhamini huyo kutoa tuzo kama hizo kwa wachezaji na makocha bora wa kila mwezi. Kwa upande wa wachezaji, Kipa wa Coastal Union ya Tanga, Ley Matampi, ndiye aliyetangazwa mshindi wa tuzo hiyo kwa Februari.

"Kimsingi ni kwamba sisi kama wadhamini wa ligi hii, tunaendelea kujivunia sana kuona ligi yenye ushindani na viwango bora vya kiuchezaji vinavyoendelea kuonekana, ndio maana utaona kwamba pamoja na ligi kuwa na wachezaji wengi wa kigeni bado wazawa wanapambana na kufanya vizuri na wanachukua tuzo hizi.

„Huu ni uthibitisho kwamba klabu zote kwa sasa zinaweza kuhudumia vema wachezaji wake kiasi cha kuweza kutoa ushindani unaotakiwa," alisema Raymond. Kwa mujibu wa Raymond, benki hiyo inaendelea na mikakati mbalimbali kuhakikisha timu hizo zinanufaika zaidi na udhamini wa benki hiyo kwenye ligi hiyo ambayo hadi sasa imetoa ajira na kipato kwa watu zaidi ya 12,000.

Aliitaja mikakati hiyo kuwa ni pamoja na mikopo ya mabasi kwa klabu mbalimbali zinazoshiriki ligi hiyo ili kurahisha usafiri, mpango ambao unahusisha hatua kadhaa hadi kufikia kukabidhi aina hiyo ya usafiri.

"Na jitihada zetu hizi haziishii kwenye mchezo wa soka tu, bali pia michezo mingine ikiwamo gofu na riadha ambapo hivi karibuni tutazindua msimu wa mwaka huu wa NBC Dodoma Marathon inayofanyika kila mwaka jijini Dodoma ambapo tumekuwa tukikusanya fedha kwa ajili ya elimu na matibabu ya saratani ya shingo ya kizazi, (marathi) ambayo yanachangia kwa kiasi kikubwa vifo vya kina mama." alisema.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa Benki ya NBC, David Raymond (kushoto), akikabidhi tuzo maalum kwa Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, baada ya kutangazwa kocha bora wa Ligi Kuu ya Soka ya Tanzania Bara, NBC Premiere League kwa mwezi Februari, mbali ya hiyo tuzo kocha huyo pia alikabidhiwa hundi ya fedha kiasi cha Sh. milioni moja kutoka kwa mdhamini huyo. Makabidhiano ya zawadi hizo yalifanyika muda mfupi kabla ya kuanza kwa mchezo kati ya Azam FC na Yanga, uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na kumaliza kwa kocha huyo kushuhudia timu yake ikichezea kichapo cha mabao 2 -1. **MPIGAPICHA WETU**

# 5,000 kushiriki Bunge Marathon 2024

**Na Faustine Feliciane**

JUMLA ya wakimbiaji 5000 kutoka katika makundi tofauti wanatarajiwa kushiriki mbio za Marathon zinazoandaliwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeelezwa.

Mbio hizo zinatarajiwa kufanyika Aprili 13, mwaka huu, jijini Dodoma huku zikilenga kukusanya fedha kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya jamii katika sekta ya elimu kwa kujenga shule maalum ya sekondari ya wavulana ya kidato cha tano na cha sita.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Naibu Spika, Mussa Azzan ‚Zungu', alisema mbio za mwaka huu zitakutanisha wakimbiaji kutoka katika taasisi za umma na binafsi.

„Mbio hizi zitakuwa za nusu Marathon yaani kilometa 21, kilometa 10 na kilometa tano, na kaulimbiu yetu mwaka huu ni ‚Shiriki Michezo Kwa Maendeleo ya Taifa Letu', alisema Zungu.

Aidha, alisema kila mshiriki atatakiwa kujisajili kupitia tovuti maalum ya mbio hizo ya Marathon.bunge.go.tz na kulipa gharama ya ushiriki.

„Kutakuwa na zawadi mbalimbali kwa washindi ambapo ni fedha na medali, tumepanga mshindi wa kwanza katika mbio za kilometa 21, atazawadiwa Sh. milioni tano, mshindi wa pili milioni tatu na mshindi wa tatu milioni 1.5," alisema Zungu. Alisema pia kutakuwa na zawadi ya ya Sh. 200,000 kwa watakaoshika nafasi ya nne mpaka ya 10.

Kwa upande wa kilometa 10 mshindi wa kwanza atapewa Sh. 2,000,000 mshindi wa pili Sh. milioni 1.5 na wa tatu Sh. milioni moja huku pia kukiwa na zawadi ya Sh. 100,000 kwa watakaoshika nafasi ya nne mpaka ya 10.

Kwa mbio za kilometa tano Zungu alisema mshindi wa kwanza atapewa medali na Sh. milioni 1.5, mshindi wapili Sh. milioni moja na mshindi wa tatu Sh. 500,000.

„Tunawakaribisha wadau mbalimbali kutoka taasisi na makampuni ya umma na binafsi na mtu mmoja mmoja kwa nafasi yake watuchangie kufanikisha malengo yetu," alisema Zungu.

Mbio hizo za Bunge nusu Marathon zinafanyika kwa mara ya pili baada ya kuanza mwaka jana

# Ruvu Shooting sasa hali tete Championship

**Na Adam Fungamwango**

KILICHOBAKI sasa ni kudura za Mwenyezi Mungu tu ili Ruvu Shooting kujinusuru isishuke daraja, baada ya juzi kukubali kipigo kikali cha mabao 7-0 dhidi ya Biashara United, katika mechi ya raundi ya 25 ya Ligi ya Champioship, mchezo ukipigwa Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara.

Matokeo hayo yanaifanya timu hiyo ambayo ilishuka daraja msimu uliopita kubaki na pointi zake 11, ikiburuza mkia, ikiwa imeshinda mechi mbili tu mpaka sasa, sare tano na kupoteza michezo 18 mpaka sasa.

Timu hiyo iliyobakisha michezo mitano tu kabla ya kuhitimisha mechi zake 30 msimu huu, ipo kwenye uwezekano mkubwa wa kushuka hadi Daraja la Pili ‚First League' msimu ujao, ikiwa imecheza Championship kwa msimu mmoja tu baada ya kushuka kutoka Ligi Kuu.

Mabao ya Biashara United yalifungwa na Zuberi Malila, alipiga mawili, Cyprian Kipenye, Rehani Kibingu, Boban Zirintusa, Vedastus Masinde na Januari Benson.

# Mieleka kufurushana Kombe la Muungano

**Na Shufaa Lyimo**

SHIRIKISHO la Mchezo wa Mieleka Tanzania (TAWF), limezitaka klabu zote kuhakikisha zinafanya mazoezi ya kutosha kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Kombe la Muungano yanayotarajiwa kuanza Mei 8 -13, mwaka huu, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Rais wa Shirikisho hilo, Andrew Kapelela, alisema mashindano hayo yatashirikisha klabu mbalimbali kutoka mikoa ya Tanzania Bara.

„Maandalizi yanaendelea vema kuelekea kwenye mashindano hayo, tunasisitiza klabu zote zifanye mazoezi", alisema Kapelela na kuongeza kuwa lengo la mashindano hayo ni kuuenzi Muungano Tanzania pamoja na kuthamini juhudi zlizofanywa na viongozi waliopitia.

Katika hatua nyingine, aliwataka Watanzania wajiunge na mchezo huo kwani ni wa kawaida kama ilivyo michezo mingine

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MALEN AWANIWA LIVER**
LIVERPOOL imeungana na Arsenal na Manchester United kuonesha nia ya kumnunua winga wa Borussia Dortmund na Uholanzi, Donyell Malen, 25. **(Bild)**

**MAGUIRE NA WEST HAM**
KOCHA wa West Ham, David Moyes, anapanga ofa mpya msimu wa majira ya joto ya kumnunua kiungo wa kati wa Manchester United, Harry Maguire, 31. **(Sun)**

**RASHFORD KUHAMIA PSG**
MSHAMBULIAJI wa England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 26, anatazamiwa kugoma kuhamia Paris St-Germain na kusalia Manchester United. **(Sun)**

**GREENWOOD AULIZIWA ATLE**
KLABU ya Atletico Madrid imeuliza kuhusu uhamisho wa mshambuliaji wa England, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 22, lakini Manchester United wameweka dau la pauni milioni 50. **(Football Transfers)**

**YORO AITAKA MADRID**
MCHEZAJI anayelengwa na Chelsea, Leny Yoro, anataka kujiunga na Real Madrid, ingawa Lille wanataka euro milioni 100 kwa mlinzi huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 18. **(Marca)**

**NEWCASTLE KUUZA WACHEZAJI**
KLABU ya Newcastle United italazimika kumuuza mmoja wa wachezaji wao muhimu msimu huu wa majira ya joto katika juhudi za kusawazisha vitabu vyao vya kuuza na kununua. **(Football Insider)**

**ERIKSEN KUONDOKA UNITED**
CHRISTIAN Eriksen ataondoka Manchester United mwishoni mwa msimu huu ikiwa ofa inayofaa itapatikana kwa kiungo huyo wa kati wa Denmark mwenye umri wa miaka 32. **(Footbal Transfers)**

**NELSON AFUATILIWA ARSENAL**
KLABU ya Brighton inamfuatilia winga wa Arsenal, Reiss Nelson mwenye umri wa miaka 24, kabla ya uhamisho wa majira ya joto. **(Football Insider)**

**DEWSBURY-HALL ATAKIWA**
BRIGHTON pia wanaendelea kumtaka Kiernan Dewsbury-Hall wa Leicester City baada ya kushindwa katika ombi la Januari la kumnunua kiungo huyo mwenye umri wa miaka 25. **(Talksport)**

**MARTINEZ KUSAINI INTER**
KLABU ya Inter Milan ina imani kwamba mshambuliaji wa Argentina, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 26, atasaini mkataba mpya. **(Fabrizio Romano)**

**GIROUD KWENDA MAREKANI**
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 37, anataka kuhamia Los Angeles au New York, pindi mkataba wake na AC Milan utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. **(Gazzetta dello Sport)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG: HUU WAKATI WA UNITED KUBADILIKA

●●● Timu ina imani na nguvu ya kufanya mambo ya ajabu, unapoishinda Liverpool unaweza...

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag amewataka Manchester United kuutumia ushindi mnono wa Kombe la FA dhidi ya Liverpool „kama wakati“ wa kuugeuza msimu wao kuwa bora.

Mchezaji aliyetokea benchi, Amad Diallo alifunga bao la ushindi dakika ya 121 na kuwezesha ushindi wa mabao 4-3 baada ya muda wa ziada na kuifanya United kutinga nusu fainali na itacheza na Coventry katika Uwanja wa Wembley mwezi ujao.

Kikosi cha Ten Hag kimevumilia msimu wa kusikitisha, lakini bado kinaweza kumaliza kampeni kwa kutwaa taji na nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

„Huu unaweza kuwa wakati mzuri,“ alisema Ten Hag baada ya ushindi huo.

„Timu ina imani na nguvu ya kufanya mambo ya ajabu. Unapoishinda Liverpool unaweza kumshinda mpinzani yeyote.“

Ten Hag anakabiliwa na maswali kuhusu mustakabali wake baada ya kuwasili kwa mmiliki mwenza mpya Sir Jim Ratcliffe, lakini Mholanzi huyo anasema wachezaji wake walionesha ni kwa nini yeye ni mtu sahihi kwa kazi hiyo kutokana na uchezaji wao dhidi ya kikosi cha Jurgen Klopp.

„Dakika 35 za kwanza, tulionesha tena kwamba mustakabali wa timu hii ni mzuri sana,“ alisema.

„Kuna uwezo mkubwa, lazima tutoe nje na kupata uthabiti. Dakika 35 za kwanza zilipendeza sana.

„Msimu huu tuna vikwazo vingi na kila wakati tunapaswa kuzoea.“

Ten Hag pia alimsifu mshindi wa mechi, Amad, ambaye alitolewa nje kwa kadi nyekundu wakati wa kusherehekea bao lake baada ya kupata kadi ya pili kwa kuvua jezi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye alihusishwa na uhamisho wa mkopo Januari, amecheza kwa dakika 88 pekee za soka msimu huu, lakini alifanya mabadiliko makubwa kama mchezaji wa akiba wa dakika za mwisho dhidi ya Liverpool.

# SOUTHGATE HANA HOFU NA JAMES KUELEKEA EURO 2024

**LONDON, England**

GARETH Southgate ana matumaini kuwa beki wa kulia wa Chelsea, Reece James, atakuwa na nafasi ya kuthibitisha kuwa yuko fiti kabla ya Euro 2024.

Kocha huyo wa England amekataa kumuacha James, ambaye amekuwa nje ya uwanja tangu kupata jeraha la msuli wa paja dhidi ya Everton Desemba mwaka jana.

Baada ya kufanyiwa upasuaji, James sasa yuko kwenye ahueni lakini bado hajarejea kwenye mazoezi na 'The Blues'.

Kinyang'anyiro dhidi ya muda sasa kinaendelea kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ambaye anatarajia kupata nafasi yake katika kikosi cha England na kusafiri hadi Ujerumani Juni.

Licha ya kukosa muda wa kucheza, Southgate ana nia ya kubaki na matumaini na James.



Alipoulizwa kama yuko nje ya mashindano, Southgate alisema: "Hapana, hatuna tarehe kamili ya kurejea lakini tunatumai atakuwa na mechi kadhaa kabla ya Euro.

"Je, anaweza kucheza mechi saba kwenye Euro? Rekodi yake katika miaka michache iliyopita ingependekeza hapana. Lakini je, ni mchezaji wa kiwango cha juu ambaye anaweza kutoa kitu muhimu, hakuna swali.

"Kwa hiyo ndio tena ni mtu mwingine ambaye hatua ya kwanza ni kurejea kwenye mazoezi, na arudi kwenye timu."

Daktari wa upasuaji wa James, Lasse Lempainen, aliliambia gazeti la The Telegraph kwamba atakuwa na hali nzuri kabla ya michuano ya Ulaya.

Hata hivyo, kocha wa klabu hiyo Mauricio Pochettino amesita kuweka tarehe ya kurejea kwake.

Huku mechi za kirafiki zikiwa zimesalia dhidi ya Brazil na Ubelgiji, macho yote sasa yataelekezwa kwa Southgate anapojaribu kuimarisha chaguo lake la mwisho kabla ya Euro 2024.

## Xavi ahofia ya Pedri kumkuta Cubarsi

**BARCELONA, Hispania**

XAVI Hernandez ametoa wito kwa Timu ya Taifa ya Hispania kuwa makini na muda wa mechi wa Pau Cubarsi ili yasimkute kama ya Pedri.

Cubarsi mwenye umri wa miaka 17, amekuwa mchezaji wa kikosi cha kwanza wa Barcelona tangu mwanzoni mwa mwaka, akivutia sana katika michezo yake tisa katika mashindano yote hadi sasa.

Beki huyo wa kati amevutia kiasi kwamba aliitwa kwenye kikosi cha wakubwa cha Hispania na kocha, Luis de le Fuente kwa ajili ya mechi zijazo za kimataifa za mwezi huu.

Ingawa mafanikio ya Cubarsi katika soka ya wakubwa yamekuwa ya kusisimua, pia yameleta ulinganisho unaotia wasiwasi na mwaka wa kwanza wa kiungo wa Barcelona Pedri katika mipangilio ya Barcelona na Hispaani.

Kwa sababu ya Euro 2020 na Olimpiki ya majira ya joto kuwa ndani ya mwaka huo huo, kiungo huyo mahiri alishiriki katika mashindano nane kwa klabu na nchi - akicheza michezo 75 kwa jumla kati ya 2020 na 2022.


Mzigo huo mkubwa wa kinda huyo umeonekana na wengi kuwa sababu kuu ya Pedri tangu wakati huo kuhangaika kuwa fiti, akiuguza majeraha nane tofauti ya nyama za paja - likiwamo moja ambalo limemweka nje hivi karibuni.

Akizungumzia kuhusu kuitwa kwa Cubarsi kikosi cha Hispania, Xavi alielezea wasiwasi wake juu ya athari ambazo mzigo kama huo unaweza kuwa nao kwa beki huyo.

"Nina furaha sana kwamba anaenda na timu ya wakubwa. Anastahili. Anacheza kwa kiwango cha juu sana," alisema Xavia.

"Natumaini 'kesi ya Pedri' haitarudiwa, lakini si jambo ninaloweza kuamua. Anastahili kwenda na timu ya taifa, yuko kwenye kiwango cha juu. Ni lazima pia tuthamini ushujaa wa De la Fuente."

Beki huyo alianza kuichezea Barca kwa mara nyingine Jumapili jioni katika mechi ya 'Blaugrana' na wenzake waliofuzu robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye Uwanja wa Civitas Metropolitan.



## Giroud kumfuata Messi Marekani

**MILAN, Italia**

MSHAMBULIAJI wa AC Milan, Olivier Giroud ana nia ya kutaka kuhamia Ligi Kuu ya Marekani (MLS), mwishoni mwa msimu huu, iwapo klabu hiyo ya Italia haitaongeza mkataba wake, kwa mujibu wa ESPN.

Giroud mwenye umri wa miaka 37, ndiye mfungaji bora wa muda wote wa Ufaransa akiwa na mabao 56.

Ametumia miaka mitatu iliyopita akiwa Milan, ambayo aliisaidia kushinda taji la Serie A mwaka 2022. Fowadi huyo angependelea kusalia kwa msimu zaidi pale Milan baada ya kuendeleza kiwango chake cha kupachika mabao msimu huu akiwa na mabao 12 katika mechi 25 za ligi, lakini anatamani kuhamia MLS ikiwa hilo haliwezekani.

Chanzo kiliiambia ESPN kwamba Giroud angependa kujiunga na Franchise kama vile njia iliyochukuliwa na mchezaji mwenzake wa zamani wa Ufaransa, Hugo Lloris ambaye alijiunga na LAFC Desemba.

Giroud amewahi kufurahia muda mzuri wa kucheza pale Arsenal na Chelsea, pamoja na klabu za Ufaransa.

Katika ngazi ya kimataifa, alinyanyua Kombe la Dunia la 2018 akiwa na Ufaransa. Pia aliiwakilisha nchi katika michuano mingine miwili ya Kombe la Dunia na michuano mitatu ya Ulaya.



HABARI MICHEZO

# CHANGALAWE AMCHAPA SALAH, ATINGA ROBO ALL-AFRICAN GAMES

**Na Saada Akida**

BONDIA wa Timu ya Taifa ya Tanzania wa Ngumi za Ridhaa, Yusuf Changalawe, ametinga robo fainali ya Michezo ya Afrika (All-African Games), inayoendelea nchini Ghana baada ya kumshinda Abdelgawwad Orabi Salah wa Misri kwa pointi.

Pambano hilo la uzito wa Light Heavy lililopigwa Jumapili usiku katika Ukumbi wa Bukom Arena jijini Accra, Ghana, lilishuhudiwa Changalawe akiibuka mshindi dhidi ya Salah ambaye ni bingwa mtetezi katika uzito huo kwenye michuano ya All-African Games, baada ya kuibuka kidedea mashindano yaliyopita ambayo yalifanyika Rabat, Morocco mwaka 2019.

Kwa ushindi huo, Changalawe pia atakuwa amelipa kisasi kwani Salah ndiye aliyemshinda kwa pointi katika michezo ya kuwania kufuzu Olimpiki ya Paris 2024 kwa Bara la Afrika walipokutana katika pambano la fainali Septemba mwaka jana katika Uwanja wa Dakar Arena mjini Dakar, Senegal.

Katika pambano la juzi Changalawe alicheza pambano lake kwa ustadi wa hali ya juu sana na kusikiliza vizuri maelekezo ya walimu wake, hivyo kumthibiti mpinzani wake huyo ambaye ameshafuzu kushiriki mashindano ya Olimpiki ya Paris 2024 kwa mara yake ya pili baada ya Olimpiki ya Tokyo, Japan 2020.

Baada ya Mtanzania huyo kutangazwa kuwa mshindi na atakutana na bondia kutoka Equatorial Guinea katika hatua ya robo fainali ya mashindano hayo yanayoendelea jijini Accra.

Changalawe anakuwa bondia wa pili kutoka Tanzania kutinga hatua hiyo baada ya Ezra Paulo aliyempiga na kumuondoa mashindanoni William Mohamed wa Shelisheli kwa RSC (Refa Kusimamisha Pambano).

Kwa mabondia wa kike, Zulfa Macho, alipoteza kwa pointi katika robo fainali dhidi ya Gisele Nyembo wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), kwenye uzito wa Fly.

Zulfa anakuwa bondia wa tatu wa Tanzania kuondoshwa kwenye michuano hiyo baada ya Abdallah Mfaume 'Nachoka' aliyetolewa na Gerald Kabinda wa Zambia kwa pointi katika uzito wa Welter, hatua ya 16-Bora na Abdallah Abdallah 'Katoto' aliyetolewa na Wibshet Bekele wa Ethiopia kwenye hatua hiyo.

Katoto aliongoza vizuri katika pambano lake hadi raundi ya mwisho, lakini hakuweza kumaliza mchezo huo wa uzani wa Fly Weight Kg 51 baada ya kuvunjika mkono na kukimbizwa moja kwa moja hospital kwa ajili ya matibabu.

# Aziz Ki bado amburuza Fei Toto takwimu Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na kufunga bao la pili dhidi ya Yanga juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kufikisha mabao 13 sawa na kiungo mshambuliaji raia wa Burkina Faso, Stephane Aziz Ki, bado Feisal Salum ‚Fei Toto', amezidiwa kwa ‚asisti' (pasi ya mwisho) ya bao.

Fei Toto amefikisha jumla ya mabao 13 akiwa sawa na Aziz Ki, wote wawili walionekana kwenye mchuano mkali wa mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Baada ya mechi ya juzi, takwimu zinaonyesha kuwa pamoja na kuwa na idadi sawa ya mabao, Aziz Ki ana ‚asisti' saba, huku Fei Toto akiwa nazo tano.

Kiungo mshambuliaji huyo wa Yanga alifunga bao lake la 13, Alhamisi iliyopita, likiwa bao pekee timu yake ikiifunga Geita Gold 1-0, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, na kwenye mchezo wa juzi, alifikisha ‚asisti' yake ya saba kwenye Ligi Kuu, akimpa pasi ya bao Clement Mzize aliyefunga bao la kufutia machozi, akiwa amechangia jumla ya mabao 20 mpaka sasa.

Mchezaji huyo pia amecheza mechi tatu pungufu ya Fei Toto, akishuka uwanjani mara 17, akicheza kwa dakika 1,305.

„Ninafunga mabao kwa ajili ya timu yangu, siwazii sana ufungaji bora, mimi kwa nafasi yangu nahesabiwa kufanya kazi ya kuifanya timu kuibuka na ushindi, ila kama itatokea mwishoni sawa," alisema Aziz Ki. Kwa upande wa Fei Toto, mpaka sasa ana ‚asisti' tano, akiwa ameisaidia Azam FC kupata mabao 18, akicheza jumla ya mechi 20, akikipiga kwa dakika,1632.

„Mimi sishindani na mtu, nacheza kwa kuisaidia Azam kutimiza malengo yake, halafu huko mwisho ndiyo tunapiga mahesabu nani ana mabao mengi, ‚asisti' na kila kitu," alisema Fei Toto baada ya mechi ya juzi ambayo Azam iliichapa Yanga mabao 2-1 Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.




# Gamondi na hali ya Pacome, Yao mechi Mamelodi

INATOKA UK. 24

zenye uwezo mkubwa wa kufunga mabao.

"Tulicheza mpira kwa ufanisi, tumeweza kuyatendea haki maboksi mawili, la mpinzani wetu na letu, tulicheza kwa kuwaheshimu Yanga kwa kuzuia ili wasipate nafasi ya kuongeza bao, baada ya kufunga la kwanza, lakini tutumie vizuri boksi lao kwa kupitisha mipira yote tulifanikiwa," alisema Dabo.

Naye Fei Toto ambaye alikuwa mwiba mchungu kwa Yanga, alisema walifuata maelekezo na kucheza mechi hiyo kwa nidhamu kubwa kwa kuwaheshimu wapinzani wao.

"Yanga ni timu kubwa, lakini tulitaka kuonyesha kuwa na sisi ni wakubwa kwa kucheza mchezo wa kikubwa. Nina waheshimu Yanga timu iliyonitoa mbali hadi kujulikana kwa hali hiyo niliwaomba msamaha baada ya kuwafunga.

"Hilo si mimi tu, hata wachezaji Ulaya tunaona mchezaji anapoifunga timu iliyomtoa mbali na kumpa jina hufanya nilichokifanya mimi, sina tatizo na mtu, ninawapenda Yanga," alisema Fei Toto.

# Simba, Yanga kuvaana Z'bar

INATOKA UK. 24

wa michuano hiyo.

Hata hivyo, alisema timu hizo zitacheza kwa mtindo wa mtoano na fainali itachezwa siku ya kilele cha sherehe za Muungano Aprili 26, mwaka huu.

Wakati huo huo, mabingwa wa Kombe la FA kwa Tanzania Bara, Yanga, watakipiga mechi ya 16 bora ya kombe hilo dhidi ya Dodoma Jiji, Aprili 10 kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, huku Simba ikipelekwa Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma kucheza dhidi ya Mashujaa, Aprili 9.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa jana mchana na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Azam FC yenyewe itakuwa nyumbani, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kucheza dhidi ya Mtibwa Sugar.

Hata hivyo, wakati TFF ikitoa ratiba hiyo, kalenda ya CAF inaonyesha kuwa timu hizo zitakuwa ugenini Aprili 5 kucheza mechi zao za marudiano, robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba ikiwa Cairo nchini Misri kucheza na Al Ahly, Yanga ikiwa Afrika Kusini kurudiana dhidi ya Mamelodi Sundowns.

Ratiba ya raundi ya nne ya Kombe la FA inaonyesha kuwa mechi hizo zitaanza Aprili 2 wakati Namungo itakapokuwa nyumbani, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi dhidi ya Kagera Sugar, Aprili 3 kwenye Uwanja wa Nyankumbu, Geita kutakuwa na mechi kati ya Geita Gold dhidi ya Rhino Rangers, huku Aprili 4 kukiwa na mchezo kati ya Singida Fountain Gate dhidi ya Tabora United, Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza.

Michezo
Jumanne Machi ... 4
Nipa...

Ten Hag: Huu wakati wa United kubadilika UKURASA 21





Pacome Yao

# GAMONDI NA HALI YA PACOME, YAO MECHI MAMELODI

●●●Ni baada ya kuumia wakichezea kichapo kwa Azam FC, pia asema Aucho sasa...

**Na Saada Akida**

LICHA ya kupoteza pointi tatu mbele ya Azam FC juzi katika mechi ya Ligi Kuu Bara kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameweka pembeni kipigo hicho na sasa jicho lake lipo katika mechi ijayo ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Katika mchezo huo wa juzi, Azam FC ilishinda mabao 2-1, huku lile la ushindi likiwekwa nyavuni na kiungo mshambuliaji wa zamani wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto', dakika ya 51, na baada ya hapo akawaomba radhi mashabiki wa timu hiyo.

Hata hivyo, Yanga ilipata pigo kuelekea mechi dhidi ya Mamelodi itakayopigwa Machi 30, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, baada ya winga wao, Pacome Zouzoua na beki wa kulia, Kouassi Attohoula Yao, kupata majeraha na kushindwa kuendelea na mchezo.

Baada ya kukamilika kwa mchezo huo, Gamondi alisema mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa na amewapoteza wachezaji wake wawili.

„Tumeongeza wachezaji majeruhi baada ya kulazimika kumtoa Pacome na Attohoula Yao ambao waliumia.

„Wachezaji hao wako chini ya uangalizi na bado hatujapata taarifa juu ya majeraha yao, tumepoteza mechi na tunarejea katika uwanja wetu wa mazoezi kuangalia tulipokosea," alisema kocha huyo.

Kuhusu hali ya kiungo wao, Khalid Aucho, Gamondi alisema nyota huyo anaendelea vizuri na matarajio yake ni kuonekana katika mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundowns.

Alisema Aucho anaendelea vizuri na ameshaanza mazoezi mapesi akiwa gym chini ya uangalizi na baada ya muda mfupi atarejea uwanjani kufanya mazoezi ya ushindani na mechi ya kimataifa anaweza kuwa sehemu ya kikosi.

"Natarajia Aucho atakuwa sehemu ya kikosi katika mchezo wetu ujao, kwa sababu tayari ameshaanza mazoezi mepesi, lakini tunasubiri taarifa kutoka kwa daktari juu ya asilimia ya kupona kwake na kuweza kucheza mechi hiyo ya ushindani," alisema Gamondi.

Akizungumzia maandalizi ya mchezo dhidi ya Mamelodi, alisema amewapa mapumziko mafupi wachezaji wake kwa sababu tangu walipomaliza mechi ya hatua ya makundi dhidi ya Al Ahly hawajapata muda wa kupumzika.

Gamondi alisema baada ya mapumziko mafupi watarejea uwanjani kujiandaa na mchezo dhidi ya Mamelodi ambao ni timu yake ya zamani ambayo aliwahi kuifundisha.

Kuhusu mchezo dhidi ya Azam, Gamondi alisema walifanya makosa katika boksi lao na Azam FC kufanikiwa kusawazisha na kipindi cha pili kutumia nafasi waliyoitengeneza kufunga bao la pili ambalo alidai halikuwa sahihi kwa kuwa lilikuwa la kuotea ‚offside'.

"Bao la pili halikuwa sahihi, mfungaji aliotea 'Offside', waamuzi hili hawajaliona, lakini ndio mpira ulivyo," alisema.

Kwa upande wa Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema taarifa juu ya ukubwa wa majeraha na muda gani watakuwa nje ya uwanja Pacome aliyeumia goti na Attohoula enka (kifundo cha mguu), itajulikana kesho baada ya kupata vipimo.

"Ni kweli Pacome na Attohoula walishindwa kumaliza mchezo kwa sababu ya kuumia ambapo mmoja aliumia goti na mwingine enka, kwa taarifa za daktari bingwa hadi saa 72 baada ya mchezo wetu dhidi ya Azam FC," alisema Kamwe.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Youssouph Dabo, alisema mchezo ulikuwa wa ushindani na zimekutana timu mbili

INAENDELEA UK. 23

# Simba, Yanga kuvaana Zanzibar

**Hawa Abdallah, ZANZIBAR na**

**Adam Fungamwango, DAR**

MIAMBA ya soka nchini, Simba na Yanga huenda ikakutana kwenye michuano ya Kombe la Muungano inayotarajiwa kuanza kutimuwa vumbi Aprili 23, mwaka huu, katika Uwanja wa Amaan visiwani hapa, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe visiwani Zanzibar jana, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Hussein Ahmada Vuai, alisema kwa kuanzia watakuwa na timu nne, mbili kutoka Tanzania Bara na mbili kutoka Zanzibar.

"Ni kweli Kombe la Muungano limerejea na kuanzia tutaanza na klabu nne, mbili kutoka Tanzania Bara na mbili kutoka visiwani Zanzibar," alisema Vuai.

Alizitaja klabu hizo kuwa ni Simba na Yanga kwa Tanzania Bara na KMKM na KVZ kwa upande wa Zanzibar.

Hata hivyo, alisema kuwa kwa msimu huu wameanza na timu hizo, lakini mwakani wanatarajia kuongeza timu na kufikia nane, ambapo kila upande utatoa timu nne.

"Mara hii tumeanza na timu hizo kutokana na ratiba kuwabana kwa kila upande ambapo wenzetu kutoka Tanzania Bara wanakabiliwa na mashindano ya kimataifa pamoja na kuwapo kwa AFCON kuliathiri ratiba za ligi na kuwa na viporo vingi," alisema.

Alisema zipo changamoto nyingine, lakini kubwa hasa ubanaji wa ratiba uliotakana na timu hizo kufika mbali Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema vigezo ambavyo wamevitumia katika kuzipata timu hizo ni kuchukuwa mshindi wa kwanza na wa pili wa msimu uliopita wa Ligi Kuu Bara na Visiwani na kwamba ratiba kamili itatolewa ili kujua nani atacheza na nani ikiwa ni pamoja na kutangaza zawadi na mdhamini

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >